# MKATABA

WA

# UMOJA WA MATAIFA

NA

# SHERIA

ZA

# MAHAKAMA YA KIMATAIFA

Idara ya Habari

# MKATABA

wa

# UMOJA WA MATAIFA

na

# SHERIA

za

# MAHAKAMA YA KIMATAIFA

Umoja wa Mataifa, New York

## UTANGULIZI

Mkataba wa Umoja wa Mataifa ulitiwa saini tarehe 26 Juni 1945, mjini San Fransisco, Marekani, mwishoni mwa mkutano kuhusu Umoja wa Mataifa. Mkataba huo ulianza kutumika tarehe 24 Oktoba 1945. Sheria ya Mahakama ya Kimataifa ni sehemu ya Mkataba huo.

Marekebisho ya kisheria yaliyofanywa katika Ibara za 23, 27 na 61 za Mkataba huo zilikubaliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 17 Desemba 1963 na kuanza kutumika rasmi tarehe 31 Agosti 1965.

Marekebisho zaidi ya sheria katika Ibara ya 61 yalikubaliwa na baraza hilo tarehe 20 Desemba 1971 na kuanza kutumika rasmi tarehe 24 Septemba 1973. Marekebisho ya sheria katika Ibara ya 109 yaliyokubaliwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa tarehe 20 Desemba 1965 yalianza kutumika tarehe 12 Juni 1968.

Marekebisho ya sheria katika Ibara ya 23 yanaongeza idadi ya Wanachama katika Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa kutoka Wanachama kumi na moja hadi kumi na tano. Ibara ya 27 iliyofanyiwa marekebisho imesisitiza kuwa maamuzi ya Baraza la Usalama katika utendaji wa kazi zake

yatafanyika kama yatapitishwa na kura za Wanachama tisa wa baraza hilo (ambapo zamani ilikuwa yapitishwe na kura za Wanachama saba) na katika shughuli zake nyingine zote yapitishwe na kura za Wanachama tisa (ambapo zamani ilikuwa ni Wanachama saba tu) ikiwa ni pamoja na kura za Wanachama watano wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Marekebisho katika Ibara ya 61 ambayo yalianza kutumika tarehe 31 Agosti 1965 yaliongeza idadi ya Wanachama wa Baraza la Uchumi na Jamii kutoka Wanachama 18 hadi Wanachama 27. Marekebisho yaliyofuatia katika Ibara hiyo ambayo yalianza kutumika tarehe 24 Septemba 1973 yaliongeza zaidi idadi ya Wanachama wa Baraza hilo kutoka 27 hadi 54.

Marekebisho katika Ibara ya 109 ambayo yanahusiana na aya ya kwanza (1) ya Ibara hiyo yanasisitiza kwamba mkutano mkuu wa nchi Wanachama wenye madhumuni ya kupitia tena Mkataba huo unaweza kufanyika katika tarehe na mahali ambapo Wanachama theluthi mbili wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kura moja ya Mwanachama yeyote kati ya tisa (ambapo zamani walikuwa saba) wa Baraza la Usalama la Umoja wa

Mataifa watapiga kura ya kukubaliana. Aya ya tatu (3) katika Ibara ya 109 ambayo inahusiana na kuwa na uwezekano wa kufanyika kwa mkutano mkuu wa kupitia Mkataba huo wakati wa kikao cha kumi cha kawaida cha Baraza Kuu, haikufanyiwa marekebisho. Aya hiyo inazungumzia kura ya Mwanachama yeyote kati ya Wanachama saba wa Baraza la Usalama. Aya hiyo ilifanyiwa kazi na Baraza Kuu mwaka 1955 katika kikao chake cha kawaida cha kumi na Baraza la Usalama.

**MKATABA WA UMOJA WA MATAIFA**

**SISI MATAIFA YA UMOJA WA MATAIFA TUMEAZIMIA:**

Kuokoa vizazi vijavyo kuondokana na vita na madhara yake ambavyo mara mbili katika maisha yetu vimeleta simanzi isiyoelezeka kwa binadamu na jamii; na tunatangaza imani yetu katika kujenga misingi ya haki za binadamu, utu na thamani ya mtu katika kuleta haki sawa miongoni mwa wanaume na wanawake na haki sawa kati ya mataifa makubwa na madogo; na kuweka misingi ya kuheshimu na kudumisha Mikataba na sheria za kimataifa; na

kutetea maendeleo ya jamii na ubora wa maisha katika uhuru kamili.

NA KWA MADHUMUNI HAYO:

Kujifunza uvumilivu na kuishi kwa amani kama majirani wema; na kuunganisha nguvu zetu katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa na kuhakikisha kuwa kwa kukubali misingi na kanuni za taasisi za kimataifa, nguvu za kijeshi hazitatumika kwa maslahi yetu wote; na kutumia vyombo vya kimataifa kukuza maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa watu wote.

**KWA PAMOJA TUMEAMUA KUUNGANISHA NGUVU ZETU ZOTE KATIKA KUFIKIA MALENGO HAYA:**

Hivyo, serikali zetu kupitia wawakilishi waliokutana katika mji wa San Francisco ambao wana madaraka kamili na wenye akili timamu, tumekubaliana juu ya Mkataba huu wa Umoja wa Mataifa na hapa tunaanzisha Umoja duniani unaojulikana kama Umoja wa Mataifa.

## SURA YA I
# MADHUMUNI NA KANUNI

**Ibara ya 1**

Madhumuni ya Umoja wa Mataifa ni:

1. Kudumisha amani na usalama wa kimataifa, na hivyo kuchukua hatua madhubuti za pamoja za kuzuia na kuondoa vitisho vyote vya amani, na kuzuia vitendo vyote vya uvamizi na vitendo vyote vinavyovunja amani, na kutumia njia za amani kwa kuzingatia kanuni za haki na sheria za kimataifa, kurekebisha au kutatua migogoro ya kimataifa au hali ambazo zinaweza kuvunja amani;
2. Kukuza mahusiano ya kirafiki miongoni mwa mataifa yanayozingatia misingi ya kuheshimiana, haki sawa na uhuru wa watu kuamua mambo yao wenyewe na kuchukua hatua nyingine madhubuti katika kuimarisha amani duniani;
3. Kupata mafanikio ya ushirikiano wa kimataifa katika kutatua matatizo yenye mtazamo wa kiuchumi, kijamii, kitamaduni au mtazamo wa matatizo ya kibinadamu na pia kukuza na kuhimiza hali ya kuheshimu haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa wote bila ubaguzi kwa misingi ya taifa, jinsia, lugha au dini; na

4. Kuwa mhimili wa kuchochea na kuhimiza utekelezaji wa malengo tuliyojiwekea.

**Ibara ya 2**

Umoja wa Mataifa na Wanachama wake, katika kutekeleza malengo yaliyoelezwa katika Ibara ya kwanza (1) utafanya kazi zake kufuatana na kanuni zifuatazo:

1. Umoja huu umeundwa chini ya msingi wa haki ya uhuru wa mataifa yote ambayo ni Wanachama.
2. Wanachama wote katika kuhakikisha wanapata haki sawa na faida kutokana na uanachama wao watatimiza kwa nia nzuri majukumu yote ya Mkataba huu.
3. Wanachama wote watasuluhisha migogoro yao ya kimataifa kwa njia za amani kwa kiasi kwamba amani, haki na usalama wa kimataifa havihatarishwi.
4. Wanachama wote katika mahusiano yao ya kimataifa watajizuia kutishia au kutumia nguvu dhidi ya Mwanachama mwingine au kuingilia uhuru wa nchi nyingine au kwa vyovyote vile kwenda kinyume na madhumuni ya Umoja wa Mataifa.
5. Wanachama wote watatakiwa kuupatia Umoja wa Mataifa msaada wowote katika hatua yoyote

utakaoichukua kwa mujibu wa Mkataba huu na watajizuia kutoa msaada kwa nchi yeyote ambayo Umoja wa Mataifa unaichukulia hatua.

6. Umoja wa Mataifa utahakikisha kwamba nchi ambazo siyo Wanachama wa Umoja huo zinaheshimu kanuni za Umoja huo kadiri inavyowezekana ili kudumisha amani na usalama wa kimataifa.
7. Mkataba huu hauna kipengele chochote kinachoupa Umoja wa Mataifa uwezo wa kuingilia mambo ya ndani ya nchi yoyote au kinachowataka Wanachama kuwasilisha mambo kama hayo ya nchi nyingine kwenye usuluhishi; lakini msingi huu hautakiwi kuathiri hatua za Umoja wa Mataifa wakati wa kutekeleza hatua zake kulingana na Sura ya VII ya Mkataba huu.

## SURA YA II

# UANACHAMA

### Ibara ya 3

Wanachama waanzilishi wa Umoja wa Mataifa watakuwa nchi ambazo baada ya kushiriki kwenye mkutano wa Umoja wa Mataifa juu ya kuanzisha Umoja huo huko San Fransisco au nchi ambazo kabla ya mkutano huo wa San Fransisco zilitia saini Tamko la Umoja wa Mataifa la tarehe 1 Januari 1942, zinatia saini Mkataba huu na zinauridhia kwa mujibu wa Ibara ya 110.

### Ibara ya 4

1. Uanachama katika Umoja wa Mataifa uko wazi kwa mataifa yote yanayopenda amani yanayokubali madhumuni yaliyomo katika Mkataba wa sasa na kwa maoni ya Umoja wa Mataifa yanaweza na yako tayari kutekeleza madhumuni hayo.
2. Kukubaliwa kwa taifa lolote kuwa Mwanachama wa Umoja wa Mataifa kutachukuliwa na uamuzi wa Baraza Kuu la Umoja huo baada ya kupendekezwa na Baraza la Usalama la Umoja huo.

**Ibara ya 5**

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambaye amewekewa vikwazo na Baraza la Usalama la Umoja anaweza kusimamishiwa haki zake zote za uanachama na Baraza Kuu baada ya kupendekezwa na Baraza la Usalama. Haki hizi zinaweza kurejeshwa na Baraza la Usalama.

**Ibara ya 6**

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa anayeendelea kukiuka kanuni zilizopo katika Mkataba huu anaweza kufukuzwa kutoka katika Umoja huo na Baraza Kuu baada ya kupendekezwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

## SURA YA III

# VYOMBO VYA UMOJA WA MATAIFA

**Ibara ya 7**

1. Umoja wa Mataifa umeundwa na vyombo vifuatavyo: Baraza kuu, Baraza la Usalama, Baraza la Uchumi na Jamii, Baraza la Udhamini, Mahakama ya Kimataifa na Sekretarieti.
2. Kama itaonekana kuna umuhimu vyombo kama hivyo vya ziada vinaweza kuanzishwa kwa mujibu wa Mkataba wa sasa.

**Ibara ya 8**

Umoja wa Mataifa hautaweka vizuizi kwa haki ya mwanamme au mwanamke kushiriki katika nafasi yoyote chini ya misingi ya usawa katika vyombo hivyo vya Umoja wa Mataifa.

## SURA YA IV
# BARAZA KUU

### Muundo

### Ibara ya 9

Baraza kuu linaundwa na Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa.

Kila Mwanachama atakuwa na wajumbe wasiozidi watano katika Baraza Kuu.

### Kazi na Mamlaka

### Ibara ya 10

Baraza kuu lina uwezo wa kujadili masuala au mambo yoyote chini ya Mkataba uliopo au masuala au mambo yanayohusiana na mamlaka na kazi za chombo chochote chini ya Mkataba wa sasa isipokuwa kama ilivyo katika Ibara ya 12, Baraza Kuu linaweza kutoa mapendekezo kwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa au kwa Baraza la Usalama au kwa vyombo vyote viwili juu ya suala au jambo lolote.

### Ibara ya 11

1. Baraza Kuu linaweza kufikiria kanuni za ushirikiano katika kudumisha amani na usalama

wa kimataifa ikiwa ni pamoja na kanuni zinazosimamia upunguzaji silaha na sheria zinazosimamia utengenezaji silaha na linaweza kutoa mapendekezo juu ya kanuni hizo kwa Wanachama au kwa Baraza la Usalama au kwa vyombo vyote hivyo viwili.

2. Baraza Kuu linaweza kujadili masuala yoyote yanayohusiana na udumishaji wa amani na usalama wa Kimataifa yanayowasilishwa na Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa au Baraza la Usalama au na nchi yeyote ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa kulingana na Ibara ya 35 aya ya pili (2) isipokuwa kama ilivyoelezwa katika Ibara ya 12 linaweza kutoa mapendekezo kuhusu mambo hayo nchi moja au nchi zaidi ya moja zinazohusiana na mambo hayo au kwa Baraza la Usalama au kwa pande zote. Suala lolote ambalo hatua ni lazima ichukuliwe litapelekwa kwa Baraza la Usalama na Baraza Kuu kabla au baada ya majadiliano.
3. Baraza Kuu linaweza kulitahadhalisha Baraza la Usalama kuhusu hali inayohofiwa kuhatarisha amani na usalama wa Kimataifa.
4. Mamlaka ya Baraza Kuu ambayo limepewa kwa

mujibu wa Ibara hii hayataathiri Ibara ya 10.

## Ibara ya 12

1. Wakati Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa likiwa katika utendaji wake wa kazi wa kutatua mgogoro kazi iliyopewa katika Mkataba huu, Baraza Kuu halitatakiwa kutoa mapendekezo yeyote kuhusu mgogoro huo mpaka Baraza la Usalama litakapo omba kufanya hivyo.
2. Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa idhini ya Baraza la Usalama, atalifahamisha Baraza Kuu katika kila kikao chake juu ya masuala yoyote yanayohusiana na kudumisha amani na usalama wa kimataifa yanayoshughulikiwa na Baraza la Usalama na pia ataliarifu Baraza Kuu au Wanachama wa Umoja wa Mataifa kama Baraza Kuu litakuwa halina kikao na papo hapo Baraza la Usalama litasimama kushughulikia masuala hayo.

## Ibara ya 13

1. Baraza Kuu litaanzisha uchunguzi na kutoa mapendekezo kwa madhumuni ya:
   a. Kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika nyanja za kisiasa na kuhimiza maendeleo ya sheria za kimataifa na taratibu zake.
   b. Kuendeleza ushirikiano wa kimataifa katika

nyanja za uchumi, jamii, tamaduni, elimu na afya na kusaidia kutambua haki za binadamu na uhuru kwa wote bila ubaguzi kwa misingi ya taifa, jinsia, lugha au dini.

2. Majukumu zaidi, kazi na mamlaka ya Baraza Kuu kama yalivyotajwa katika aya ya kwanza (1b) yameelezwa zaidi katika Sura ya IX na X.

## Ibara ya 14

Kulingana na masharti yaliyomo katika Ibara ya kumi na mbili (12), Baraza Kuu linaweza kutoa mapendekezo juu ya hatua za kurekebisha hali yoyote bila kujali chanzo chake inayoweza kuharibu uhusiano miongoni mwa mataifa ikiwa ni pamoja masuala yanayohusiana na ukiukwaji wa Mkataba wa sasa kama ilivyoelezwa katika madhumuni na kanuni za Umoja wa Mataifa.

## Ibara ya 15

1. Baraza Kuu litapokea na kufikiria taarifa za mwaka na taarifa maalumu kutoka kwa Baraza la Usalama. Taarifa hizo zitajumuisha hatua zilizochukuliwa au kuamuliwa na Baraza la Usalama katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa.
2. Baraza Kuu litapokea na kufikiria taarifa kutoka vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa.

**Ibara ya 16**

Baraza Kuu litafanya kazi zake kufuatana na taratibu za udhamini wa kimataifa kama itakavyopewa chini ya Sura ya XII na XIII ikiwa ni pamoja na kuidhinisha makubaliano ya udhamini kwa maeneo ambayo si muhimu.

**Ibara ya 17**

1. Baraza Kuu litaangalia na kupitisha bajeti ya Umoja huo.
2. Gharama za matumizi ya Umoja huo zitachangiwa na Wanachama wote kutokana na viwango vitakavyowekwa na Baraza Kuu.
3. Baraza Kuu litaangalia na kuidhinisha fedha na mpangilio wa bajeti za mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyotajwa katika Ibara ya 57 na kuchunguza bajeti za utawala wa mashirika hayo kwa lengo la kutoa mapendekezo kwa mashirika husika.

## Upigaji kura

**Ibara ya 18**

1. Kila Mwanachama wa Baraza kuu atakuwa na kura moja.
2. Maamuzi ya Baraza Kuu kuhusu masuala muhimu yatatolewa kwa kura ya theluthi mbili

zitakazopigwa na Wanachama wote watakaokuwepo na kupiga kura. Masuala hayo yatahusu: mapendekezo kuhusu amani na usalama wa kimataifa, uchaguzi wa Wanachama wasio wa kudumu wa Baraza la Usalama, uchaguzi wa Wanachama wa Baraza la Uchumi na Jamii, uchaguzi wa Wanachama wa Baraza la Udhamini kama ilivyoelezwa katika aya ya kwanza 'c' (1c) ya Ibara ya 86, kukubaliwa kwa Wanachama wapya wa Umoja wa Mataifa, kusimamishwa kwa haki za uanachama, kufukuzwa kwa Wanachama, masuala yahusuyo uendeshaji wa taratibu za udhamini na masuala ya bajeti.

3. Maamuzi juu ya masuala mengine ikiwa ni pamoja na uamuzi wa makundi mengine ya masuala yatakayoamuliwa na theluthi mbili ya Wanachama yatafikiwa na Wanachama walio wengi watakaokuwepo kwa kupiga kura.

## Ibara ya 19

Mwanachama wa Umoja wa Mataifa ambaye bado anadaiwa fedha za mchango wake katika Umoja huo hataruhusiwa kupiga kura katika Baraza Kuu kama kiasi cha deni lake ni sawa au linazidi kiasi cha mchango wake wa miaka miwili iliyopita. Baraza

Kuu linaweza kumruhusu Mwanachama huyo kupiga kura kama likiridhishwa kuwa sababu zilizopelekea Mwanachama huyo kushindwa kulipa michango yake ziko nje ya uwezo wake.

## Taratibu

### Ibara ya 20

Baraza Kuu litakutana katika mikutano yake ya kawaida ya mwaka na katika mikutano maalumu pale hali inapolazimu. Mikutano hiyo maalumu itaitishwa na Katibu Mkuu wa Umoja huo kufuatia ombi la Baraza la Usalama au wingi wa Wanachama wa Umoja wa Mataifa.

### Ibara ya 21

Baraza Kuu litajiwekea kanuni na taratibu zake. Na litamchagua Rais wake kwa kila kikao chake.

### Ibara ya 22

Baraza Kuu linaweza kuongeza vyombo vingine pale itakapoonekana kwamba vyombo hivyo ni muhimu katika utendaji wa kazi zake.

## SURA YA V

# BARAZA LA USALAMA

### Muundo

### Ibara ya 23

1. Baraza la Usalama linaundwa na Wanachama 15 wa Umoja wa Mataifa. Jamhuri ya watu wa China, Ufaransa, Urusi, Uingereza, Ireland kaskazini na Marekani ni Wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Baraza Kuu litachagua Wanachama wengine kumi wa Umoja wa Mataifa kuwa Wanachama wasio wa kudumu wa Baraza la Usalama. Uchaguzi huu utatokana kwanza na mchango wa Wanachama wa Umoja wa Mataifa katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa na kwa madhumuni mengine ya Umoja huo kutegemeana na nchi hizo ziko wapi kijiografia.
2. Wanachama wasio wa kudumu katika Baraza la Usalama watachaguliwa kwa kipindi cha miaka miwili. Katika uchaguzi wa kwanza wa Wanachama wasio wa kudumu, baada ya kuongeza Wanachama wa Baraza la Usalama kutoka 11 hadi 15, Wanachama wawili kati ya wanne wa nyongeza watachaguliwa kwa kipindi

cha mwaka mmoja. Mwanachama anayemaliza muda wake haruhusiwi kuchaguliwa tena katika uchaguzi unaofuata.

Kila Mwanachama wa Baraza la Usalama atakuwa na mwakilishi mmoja.

## Kazi na Mamlaka

### Ibara ya 24

1. Ili kuhakikisha utendaji mzuri wa kazi za Umoja wa Mataifa, Wanachama wake wanajadili juu ya jukumu la Baraza la Usalama juu ya suala la kudumisha amani na usalama wa Kimataifa. Wanachama hao wanakubaliana kwamba ili kutekeleza majukumu hayo Baraza la Usalama lifanye kazi hiyo kwa niaba yao.
2. Katika kutekeleza majukumu hayo Baraza la Usalama litafanya kazi kwa mujibu wa madhumuni na kanuni za Umoja wa Mataifa. Mamlaka iliyopewa Baraza la Usalama katika utendaji wake wa kazi yameelezwa katika Sura ya VI, VII, VIII na XII.
3. Baraza la Usalama litatoa taarifa ya mwaka na pale inakapobidi taarifa maalum kwa Baraza Kuu kwa hatua zaidi.

### Ibara ya 25

Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaafikiana kukubali kutekeleza maamuzi ya Baraza la Usalama kulingana na Mkataba wa sasa.

### Ibara ya 26

Ili kuendeleza uanzishwaji na udumishaji wa amani na usalama wa kimataifa bila kutumia rasilimali nyingi kutengeneza silaha, Baraza la Usalama litakuwa na jukumu la kuunda, kwa msaada wa Kamati ya kijeshi inayozungumziwa katika Ibara ya 47, mipango itakayowasilishwa kwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa ya kusimamia taratibu za kupunguza utengenezaji wa silaha.

## Upigaji kura

### Ibara ya 27

1. Kila Mwanachama wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa atakuwa na kura moja.
2. Maamuzi ya Baraza la Usalama juu ya taratibu mbalimbali yatafikiwa na kura ya makubaliano ya Wanachama tisa.
3. Maamuzi ya Baraza la Usalama juu ya masuala mengine yatafikiwa kwa kura ya makubaliano ya Wanachama tisa zikiwemo kura za Wanachama wa kudumu kama maamuzi katika Sura ya VI na

aya ya tatu (3) ya Ibara ya 52 Mwanachama anayehusika na mgogoro hatapiga kura.

## Taratibu

### Ibara ya 28

1. Baraza la Usalama litaundwa katika namna ambayo litafanya kazi kwa muda wote. Kila Mwanachama wa Baraza la Usalama kwa madhumuni hayo atawakilishwa wakati wote Umoja wa Mataifa unapokutana.
2. Baraza la Usalama litafanya mikutano ya mara kwa mara ambayo kila Mwanachama pale inapolazimu atawakilishwa na mjumbe wa serikali yake au mwakilishi maalumu aliyeteuliwa.
3. Baraza la Usalama linaweza kuwa na mikutano mahali pengine tofauti na makao makuu ya Umoja wa Mataifa kama uamuzi huo utarahisisha kazi zake.

### Ibara ya 29

Baraza la Usalama linaweza kuunda vyombo zaidi kama itaonekana ni lazima kwa utendaji wa kazi zake.

### Ibara ya 30

Baraza la Usalama litaanzisha kanuni na sheria zake ukiwemo utaratibu wa kumchagua Rais wake.

**Ibara ya 31**

Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa ambaye si Mwanachama wa Baraza la Usalama anaweza kushiriki katika vikao vya baraza bila kupiga kura, juu ya suala lolote litakaloletwa mbele ya Baraza la Usalama pale ambapo ataona suala hilo lina maslahi ili asiathirike.

**Ibara ya 32**

Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa ambaye si Mwanachama wa Baraza la Usalama au nchi ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, kama anahusika na mgogoro ambao uko chini ya Baraza la Usalama atakaribishwa kuhudhuria, bila kupiga kura katika mjadala unaohusiana na mgogoro huo. Baraza la Usalama litaweka masharti yatakayoamua ushiriki wa nchi hiyo ambayo siyo Mwanachama wa Umoja wa Mataifa.

## SURA YA VI

# MAAFIKIANO YA KUTAFUTA AMANI PENYE MIGOGORO

### Ibara ya 33

1. Pande zinazohusika katika mgogoro ambao ukiendelea utahatarisha amani na usalama wa Kimataifa, kwanza kabisa itabidi zitafute suluhu kwa njia ya mazungumzo, uchunguzi, suluhisho, mapatanisho, hukumu ya mahakama, kuomba msaada wa suluhisho kutoka mashirika ya kikanda au mpango maalumu wa suluhisho la kikanda au njia nyingine za amani zitakazoonekana zinafaa kwa pande zote.
2. Baraza la Usalama pale litakapoona umuhimu litazitaka pande hizo kutatua migogoro yao kwa njia hizo.

### Ibara ya 34

Baraza la Usalama linaweza likachunguza mgogoro wowote, au hali yoyote itakayoweza kuleta migongano ya kimataifa au kusababisha mgogoro, ili kujua kama kuendelea kwa mgogoro au hali hiyo kunaweza kuhatarisha uimarishaji wa amani na usalama wa Kimataifa.

## Ibara ya 35

1. Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa anaweza kuwasilisha katika Baraza la Usalama au Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mgogoro au hali yoyote ya aina hiyo inayozungumziwa katika Ibara ya 34.
2. Nchi ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa inaweza kuliarifu Baraza la Usalama au Baraza Kuu mgogoro wowote ambao unaihusu kama inakubali mapema kuwa suluhu inaweza kupatikana kwa mujibu wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa.
3. Utaratibu wa Baraza Kuu katika masuala yaliyo chini ya Ibara hii yatakuwa chini ya maafikiano ya Ibara ya 11 na 12.

## Ibara ya 36

1. Baraza la Usalama katika kila hatua ya mgogoro kama inavyoelezwa katika Ibara ya 33 au hali ya namna hiyo litapendekeza hatua madhubuti au taratibu za marekebisho.
2. Baraza la Usalama litafikiria kila hatua ya maafikiano ya migogoro ambayo tayari yamekubaliwa na pande husika.
3. Katika kutoa mapendekezo chini ya Ibara hii Baraza la Usalama litafikiria pia migogoro ya

kisheria inapelekwa na pande zinazohusika kwenye Mahakamaya Kimataifa kutegemeana na maamuzi ya sheria za mahakama.

## Ibara ya 37

1. Pande zinazohusika na mgogoro wa aina hiyo inayozungumziwa katika Ibara ya 33 zikishindwa kutatua mgogoro huo kwa njia zilizoelezwa katika Ibara hiyo hazina budi kuwasilisha mgogoro huo kwa Baraza la Usalama.
2. Kama Baraza la Usalama litaona kuwa kuendelea kwa mgogoro huo kunaweza kuhatarisha udumishaji wa amani na usalama wa Kimataifa litaamua kama lichukue hatua chini ya Ibara ya 36 au litapendekeza masharti muafaka ya maafikiano yanayoonekana kufaa.

## Ibara ya 38

Bila upendeleo wowote katika maamuzi ya Ibara ya 33 hadi 37, Baraza la Usalama linaweza, kama pande zote zinazohusika na mgogoro zitaomba, kutoa mapendekezo kwa pande husika ya upatanishi katika mgogoro huo.

## SURA YA VII

# HATUA DHIDI YA VITISHO VYA AMANI, UVUNJAJI WA AMANI NA VITENDO VYA UVAMIZI

### Ibara ya 39

Baraza la Usalama litaamua kuwepo kwa vitisho dhidi ya amani, uvunjaji wa amani au vitendo vya uvamizi na litatoa mapendekeo au maamuzi juu ya hatua zitakazochukuliwa kama ilivyoamuliwa kwa mujibu wa ibara ya 41 na 42 katika kudumisha au kurejesha amani na usalama wa Kimataifa.

### Ibara ya 40

Ili kuzuia hali ya kukua kwa mgogoro, Baraza la Usalama kabla ya kutoa mapendekezo au maamuzi juu ya hatua zilizoamuliwa katika Ibara ya 39 litaziita pande zote zinazohusika ili zikubaliane na maamuzi katika Ibara ya 39 kama itaonekana ni muhimu. Hatua hizo za maamuzi zitakuwa si za upendeleo wa haki, madai au nafasi ya pande zinazohusika. Baraza la Usalama litafuatilia kwa karibu kushindwa kwa pande hizo kukubaliana na maamuzi hayo.

### Ibara ya 41

Baraza la Usalama linaweza kuamua hatua zipi ambazo hazitahusisha matumizi ya nguvu za kijeshi

zitachukuliwa katika kutoa maamuzi na kuwataka Wanachama wa Umoja wa Mataifa kuzifuata hatua hizo. Hatua hizo zinaweza kuwa ni pamoja na vikwazo kamili au vya muda vya uchumi na njia za mawasiliano kama vile za reli, usafiri wa maji, usafiri wa anga, njia za posta, redio, mawasiliano kwa njia ya simu na njia nyingine za mawasiliano na kuvunja uhusiano wa kibalozi.

## Ibara ya 42

Pale Baraza la Usalama litakapoona kwamba hatua zilizoelezwa katika Ibara ya 41 hazitoshelezi au hazifai kabisa, linaweza kuchukua hatua za kutumia majeshi ya anga, ardhini au majini pale litakapoona umuhimu wa kufanya hivyo ili kudumisha au kurejesha amani na usalama wa Kimataifa. Hatua hiyo inaweza ikajumuisha maandamano, kuwekewa vikwazo na hatua nyingine za majeshi ya anga, ya majini na ya nchi kavu ya Umoja wa Mataifa.

## Ibara ya 43

1. Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ili kushiriki katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa, watatoa kwa Baraza la Usalama kulingana na makubaliano maalumu au Mikataba, majeshi, misaada na zana ikiwa ni pamoja na kutoa haki za kupita kwa madhumuni ya

kudumisha amani na usalama wa Kimataifa.

2. Makubaliano maalum au Mikataba hiyo ndiyo itatoa ukubwa wa majeshi, uwezo wa majeshi, mahali yatakapopelekwa majeshi na aina ya misaada inayotakiwa.
3. Makubaliano maalumu au Mikataba hiyo itajadiliwa haraka iwezekanavyo baada ya kuombwa na Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa. Mikataba hiyo itatiwa saini baina ya Baraza la Usalama na Wanachama au kati ya Baraza la Usalama na makundi ya Wanachama na lazima iridhiwe na nchi zenye haki ya kutia saini kulingana na katiba za nchi zao.

## Ibara ya 44

Pale ambapo Baraza la Usalama litaamua kutumia nguvu, kabla ya kumtaka Mwanachama ambaye hakuwakilishwa katika maamuzi ya kutoa majeshi kwa mujibu wa Ibara ya 43, litamwalika Mwanachama huyo, kama atataka kushiriki katika maamuzi ya Baraza la Usalama ya kutoa majeshi.

## Ibara ya 45

Ili kuwezesha Umoja wa Mataifa kuchukua hatua za haraka za kijeshi, Wanachama watatakiwa kutoa haraka majeshi ya anga ambayo yatajiunga na kikosi cha kimataifa ili kutekeleza hatua hiyo. Nguvu na

kiwango cha utayari wa majeshi haya na mipango ya ushirikiano katika kutekeleza hatua hiyo vitaamuliwa kwa mujibu wa makubaliano maalumu au Mikataba inayozungumziwa katika Ibara ya 43 na Baraza la Usalama kwa kushirikiana na Kamati ya kijeshi.

**Ibara ya 46**

Mipango ya kutumia nguvu za kijeshi itafanywa na Baraza la Usalama kwa kushirikiana na Kamati ya Kijeshi.

**Ibara ya 47**

1. Kutakuwepo Kamati ya kijeshi kwa ajili ya kulishauri na kusaidia mahitaji ya kijeshi ya Baraza la Usalama kwa lengo la kulinda amani na usalama wa kimataifa, matumizi ya majeshi yaliyopo, matumizi ya silaha na uwezekano wa kupunguza silaha.
2. Kamati ya kijeshi itaundwa na wakuu wa majeshi ya Wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama au wawakilishi wao. Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa ambaye si mwakilishi wa kudumu wa kamati hiyo, ataalikwa na Kamati hiyo ili ashiriki katika kamati pale ambapo ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya kamati hiyo yanamuhitaji Mwanachama huyo.
3. Kamati ya kijeshi itawajibika chini ya Baraza la Usalama kwa maelekezo ya matumizi ya majeshi

yaliyoko chini ya Baraza la Usalama. Masuala yanayohusika na matumizi ya majeshi hayo yatafuata baadaye.

4. Kamati ya Kijeshi kwa kuagizwa na Baraza la Usalama na baada ya mashauriano na mashirika ya kikanda, inaweza kuanzisha kamati ndogo za kikanda.

## Ibara ya 48

1. Hatua zitakazohitajika kutekeleza maamuzi ya Baraza la Usalama kwa lengo la kudumisha amani na usalama wa kimataifa zitachukuliwa na Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa au baadhi yao kama Baraza la Usalama litakavyoamua.
2. Maamuzi hayo yatatekelezwa na Wanachama wa Umoja wa Mataifa moja kwa moja kupitia mashirika ya kimataifa ambamo ni Wanachama.

## Ibara ya 49

Wanachama wa Umoja wa Mataifa wataungana kukidhi misaada inayotakiwa katika kutekeleza hatua zilizoamuliwa na Baraza la Usalama.

## Ibara ya 50

Kama hatua za Baraza la Usalama zitachukuliwa dhidi ya nchi yeyote ile na hatua hizo zikaaathiri

nchi nyingine kiuchumi ambayo aidha ni Mwanachama wa Umoja wa Mataifa au siyo Mwanachama, nchi hiyo iliyoathirika ina haki ya kushauriana na Baraza la Usalama juu ya kutafuta suluhisho la tatizo hilo.

**Ibara ya 51**

Hakuna kilicho ndani ya Mkataba huu kitakachoathiri haki ya msingi ya mtu au ulinzi wa pamoja kama shambulio la kijeshi litafanywa dhidi ya Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, mpaka hapo Baraza la Usalama litakapochukua hatua zinazohitajika katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa. Hatua zitakazochukuliwa na nchi Wanachama katika zoezi hilo la kujilinda zitatolewa taarifa mapema kwa Baraza la Usalama na hazitaathiri kwa njia yoyote ile mamlaka na majukumu ya Baraza la Usalama chini ya Mkataba huu kama ambavyo litaona muhimu kuchukua hatua pale inapowezekana ili kudumisha au kurudisha ulinzi na usalama wa kimataifa.

# SURA YA VIII

# MIPANGO YA KIKANDA

## Ibara ya 52

1. Hakuna kilicho ndani ya Mkataba huu kinachozuia utaratibu wa kuundwa kwa mipango ya kikanda au mashirika yanayoshughulikia masuala yanayohusika na udumishaji wa amani na usalama wa kimataifa kama itaonekana ni muhimu kufanya hivyo maadam mipango ya aina hiyo inazingatia madhumuni na kanuni za Umoja wa Mataifa.
2. Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaoingia katika mipango kama hiyo au kuunda mashirika kama hayo watafanya kila juhudi ili kufanikisha utatuzi wa migogoro ya kikanda kwa kutumia utaratibu kama huo kabla ya kuipeleka migogoro hiyo kwenye Baraza la Usalama.
3. Baraza la Usalama litahimiza utatuzi wa migogoro ya kikanda kwa kutumia utaratibu kama huo wa kuunda mipango ya kikanda au mashirika yanayoshughulikia masuala yanayohusika na udumishaji wa amani na usalama wa kimataifa utakaofanywa na nchi zinazohusika au kwa kuelekezwa na Baraza la Usalama.

4. Ibara hii haizuii kwa njia yeyote ile matumizi ya Ibara ya 34 na 35.

## Ibara ya 53

1. Baraza la Usalama pale inapowezekana litatumia mipango ya kikanda au mashirika ya kikanda katika kutekeleza majukumu yake. Lakini hakuna hatua zitakazochukuliwa chini ya mipango ya kikanda au mashirika ya kikanda bila idhini ya Baraza la Usalama, isipokuwa hatua dhidi ya nchi yoyote adui kama ilivyoelezwa katika aya ya pili (2) ya Ibara hii na kufafanuliwa katika Ibara ya 107 au katika mipango ya kikanda iliyoanzishwa ili kupambana na sera za kivamizi dhidi ya nchi yoyote, hadi wakati ambapo Umoja wa Mataifa kwa ombi kutoka serikali husika utachukua hatua za kuzuia sera za kivamizi za nchi husika.
2. Neno "nchi adui" kama lilivyotumika katika aya ya kwanza (1) ya Ibara hii linamaanisha nchi yoyote ambayo wakati wa vita vya pili vya dunia imekuwa adui wa nchi yoyote iliyotia saini katika Mkataba wa sasa.

## Ibara ya 54

Baraza la Usalama katika kipindi chote litakuwa linaarifiwa juu ya shughuli ambazo zimekuwa

zikichukuliwa au zimekuwa zikifikiriwa kuchukuliwa chini ya utaratibu huu wa kikanda au chini ya utaratibu wa mashirika ya kikanda kwa madhumuni ya kudumisha amani na usalama wa kimataifa.

## SURA YA IX

# USHIRIKIANO WA KIMATAIFA WA KIUCHUMI NA KIJAMII

### Ibara ya 55

Kwa madhumuni ya kuweka mazingira ya utulivu na maendeleo vitu ambavyo ni muhimu katika kuleta amani na ushirikiano wa kirafiki miongoni mwa mataifa kwa misingi ya haki sawa na uhuru wa mataifa wa kujiamulia mambo yao wenyewe, Umoja na Mataifa utahimiza:

a. Viwango vikubwa vya maisha ya watu, ajira, na kuweka mazingira yatakayoleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii;

b. Utatuzi wa matatizo ya kimataifa ya kiuchumi, kijamii, kiafya na matatizo yanayohusiana na masuala hayo na ushirikiano wa kimataifa katika njanja za utamaduni na elimu;

c. Kuheshimu na kusisitiza haki za binadamu na uhuru wa kimsingi kwa wote bila ubaguzi kwa misingi ya taifa, jinsia, lugha au dini.

### Ibara ya 56

Wanachama wote waahidi wenyewe kuchukua hatua za pamoja au hatua za kila Mwanachama za kushirikiana na Umoja wa Mataifa kwa madhumuni ya kutekeleza malengo yaliyopo katika Ibara ya 55.

## Ibara ya 57

1. Mashirika mbalimbali maalum, yaliyoanzishwa kwa Mkataba miongoni mwa mataifa na yakawa na majukumu makubwa kimataifa kama inavyofafanuliwa katika Mikataba hiyo katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kielimu, kiafya na nyanja zinazohusiana na hizo, yatakuwa na uhusiano na Umoja wa Mataifa kwa mujibu wa Ibara ya 63.
2. Mashirika hayo yakiwa na uhusiano kama huo na Umoja wa Mataifa, yatajulikana kama mashirika maalumu ya Umoja huo.

## Ibara ya 58

Umoja wa Mataifa utatoa mapendekezo ya kuratibu sera na shughuli za mashirika hayo maalumu.

## Ibara ya 59

Umoja huo pale itakapoonekana inafaa, utaanzisha mazungumzo na mataifa yaliyohusika katika kuunda mashirika mapya maalumu yatakayohitajika katika kufanikisha madhumuni yaliyopo katika Ibara ya 55.

## Ibara ya 60

Majukumu ya utendaji wa kazi za Umoja wa Mataifa yaliyoelezwa katika Sura hii yatawekwa chini ya mkutano wa Baraza Kuu na kwa mamlaka ya Baraza Kuu Baraza la Uchumi na Jamii litakuwa na mamlaka yaliyoelezwa katika Sura ya X.

## SURA YA X

# BARAZA LA UCHUMI NA JAMII

**Muundo**

**Ibara ya 61**

1. Baraza la Uchumi na Jamii linaundwa na Wanachama hamsini na nne ambao ni Wanachama wa Umoja wa Mataifa waliochaguliwa na Baraza Kuu.
2. Kama ilivyofafanuliwa katika aya ya tatu (3), Wanachama kumi na nane wa Baraza la Uchumi na Jamii watachaguliwa kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu. Mwanachama atakayemaliza muda wake ataweza kuchaguliwa tena katika uchaguzi unaofuata.
3. Katika uchaguzi wa kwanza baada ya kuongeza idadi ya Wanachama wa Baraza la Uchumi na Jamii kutoka ishirini na saba hadi hamsini na nne, ikiwa ni nyongeza ya Wanachama waliochaguliwa kuchukua nafasi za Wanachama tisa ambao kipindi chao cha kazi kinaisha ifikapo mwisho wa mwaka unaohusika, Wanachama ishirini na saba wengine watachaguliwa. Kati ya Wanachama hao ishirini na saba wengine, kipindi

cha kazi cha Wanachama tisa waliochaguliwa kitakwisha baada ya mwaka mmoja, na kipindi cha kazi cha Wanachama wengine tisa kitakwisha baada ya miaka miwili kulingana na utaratibu uliowekwa na Baraza Kuu.

4. Kila Mwanachama wa Baraza la Uchumi na Jamii atawakilishwa na mjumbe mmoja.

## Kazi na Mamlaka

### Ibara ya 62

1. Baraza la Uchumi na Jamii linaweza kufanya au kuanzisha uchunguzi na taarifa kuhusu masuala ya kimataifa ya kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kielimu, kiafya na mambo mengine yanayohusiana na masuala hayo na linaweza kutoa mapendekezo kuhusiana na suala lolote kwenye Baraza Kuu, kwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa na kwa mashirika maalumu husika.
2. Linaweza kutoa mapendekezo yenye lengo la kuendeleza haki za binadamu na uhuru wa msingi kwa wote.
3. Linaweza kutayarisha miswada ya Mikataba itakayowasilishwa kwenye Baraza Kuu kuhusu masuala yaliyo chini yake.
4. Linaweza kuitisha, kulingana na kanuni za Umoja

wa Mataifa, mikutano ya kimataifa kuhusu masuala yaliyo chini yake.

## Ibara ya 63

1. Baraza la Uchumi na Jamii linaweza likafanya makubaliano na mashirika yaliyotajwa katika Ibara ya 57, yanayofafanua misingi ya ushirikiano kati ya mashirika yanayohusika na Umoja wa Mataifa. Makubaliano kama hayo yatathibitishwa na Baraza Kuu.
2. Linaweza kuratibu shughuli za mashirika maalumu kwa kuwa na mashauriano na mapendekezo kwa mashirika hayo na kwa kutoa mapendekezo kwa Baraza Kuu na kwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa.

## Ibara ya 64

1. Baraza la Uchumi na Jamii litachukua hatua zinazofaa kupata taarifa za kawaida kutoka kwa mashirika maalum. Linaweza kufanya mipango na Wanachama wa Umoja wa Mataifa na Mashirika maalum katika kupata taarifa juu ya hatua zilizochukuliwa kutekeleza mapendekezo yake na mapendekezo juu ya masuala yaliyopo chini yake yaliyofanywa na Baraza Kuu.
2. Linaweza kuwasiliana na Baraza Kuu kuhusu maoni yake juu ya taarifa hizo.

## Ibara ya 65

Baraza la Uchumi na Jamii linaweza kulipatia taarifa Baraza la Usalama na linaweza kulisaidia Baraza hilo kama litaomba kufanya hivyo.

## Ibara ya 66

1. Baraza la Uchumi na Jamii litafanya kazi zake zilizo chini ya uwezo wake pamoja na kutekeleza mapendekezo ya Baraza Kuu.
2. Linaweza, kwa idhini ya Baraza Kuu, kutoa huduma baada ya kuombwa na Wanachama wa Umoja wa Mataifa na Mashirika maalum.
3. Linaweza kufanya kazi nyinginezo kama zilivyoelezwa katika Mkataba huu au itakazopewa na Baraza Kuu.

## Upigaji Kura

## Ibara ya 67

1. Kila Mwanachama wa Baraza la Uchumi na Jamii atakuwa na kura moja.
2. Maamuzi ya Baraza la Uchumi na Jamii yatafikiwa na Wanachama wengi waliopo na waliopiga kura.

**Taratibu:**

**Ibara ya 68**

Baraza la Uchumi na Jamii litaunda kamati katika sekta za Uchumi na Jamii kwa madhumuni ya kudumisha haki za binadamu na kuunda kamati ambazo zitahitajika katika kufanikisha kazi zake.

**Ibara ya 69**

Baraza la Uchumi na Jamii litamkaribisha Mwanachama yeyote wa Umoja wa Mataifa kushiriki bila kupiga kura katika majadiliano juu ya suala lolote linalomhusu Mwanachama huyo.

**Ibara ya 70**

Baraza la Uchumi na Jamii linaweza kufanya mipango ya kuruhusu wawakilishi wa mashirika maalum kushiriki bila kupiga kura katika majadiliano ya Baraza na kushiriki katika majadiliano ya tume mbalimbali zilizoundwa na Baraza hilo na wajumbe wa Baraza hilo kushiriki katika majadiliano ya mashirika maalum.

**Ibara ya 71**

Baraza la Uchumi na Jamii linaweza kufanya mipango ya majadiliano na mashirika yasiyo ya kiserikali ambayo yanahusika na masuala yaliyo chini ya Baraza hilo. Mipango hiyo inaweza ikafanywa

na mashirika ya Kimataifa na pale inapofaa na mashirika ya kitaifa baada ya mashauriano na Wanachama husika wa Umoja wa Mataifa.

**Ibara ya 72**

1. Baraza la Uchumi na Jamii litafuata kanuni na sheria zake ukiwemo utaratibu za kumchagua rais wake.

2. Baraza la Uchumi na Jamii litakutana kama inavyotakiwa kwa mujibu wa kanuni zake, ambazo zinajumuisha makubaliano au sheria za kuitisha mikutano kwa ombi maalum kutoka kwa Wanachama wake walio wengi.

## SURA YA XI

# TAMKO KUHUSU NCHI ZISIZOJITAWALA ZENYEWE

### Ibara ya 73

Wanachama wa Umoja wa Mataifa ambao wana majukumu ya utawala wa nchi ambazo watu wake hawaJajitawala wenyewe kikamilifu, wanatambua msingi kwamba watu hao ni muhimu na wanakubali jukumu la kuendeleza kwa kiwango kikubwa amani na usalama wa kimataifa kama inavyosisitizwa katika Mkataba huu, kuendeleza wananchi wa nchi hizo kwa madhumuni haya;

a. Kuhakikisha kwamba watu wa nchi hizo wanapewa heshima zao katika kuendelezwa kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu na wanapata haki sawa na wanalindwa kutokana na kunyanyaswa.
b. Kuwaendeleza ili wajitawale wenyewe kulingana na matakwa yao kisiasa na kuwasaidia kupata vyombo huru vya kisiasa kulingana na hali halisi ya nchi hizo, watu wake na maendeleo yao.
c. Kuendeleza amani na usalama wa Kimataifa.
d. Kuendeleza hatua muhimu za maendeleo, kuhimiza utafiti na ushirikiano miongoni mwa

nchi hizo na pale inapoonekana inafaa ushirikiano na mataifa maalumu ya kimataifa kwa madhumuni ya kupata maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kisayansi kama inavyoelezwa katika Ibara hii.

e. Kuwasiliana na Katibu Mkuu kwa madhumuni ya kupeleka habari zinazohusu usalama na mambo ya kikatiba, takwimu na habari nyingine zinazohusu hali ya uchumi, jamii, elimu katika nchi hizo ambazo ziko chini yao isipokuwa kwa zile nchi ambazo zimeelezwa katika Sura ya XII na XIII.

## Ibara ya 74

Wanachama wa Umoja wa Mataifa pia wanakubaliana kuwa msingi wa sera zao kwa nchi hizo zinazotajwa katika Sura hii, kama zilivyo sehemu nyingine za mijini katika nchi hizo, uwe wa ujirani mwema na umuhimu mkubwa uwekwe katika mambo yanayohusu maendeleo ya kijamii, kiuchumi na kibiashara kama ilivyo duniani kote.

## SURA YA XII

# UTARATIBU WA UDHAMINI WA KIMATAIFA

### Ibara ya 75

Umoja wa Mataifa utaanzisha, chini ya mamlaka yake, utaratibu wa udhamini wa Kimataifa utakaotawala na kusimamia nchi kama hizo kutokana na Mikataba inayowekwa kati ya nchi hizo na utaratibu huo. Kutokana na Mikataba hiyo nchi hizo zitaitwa nchi zilizodhaminiwa.

### Ibara ya 76

Shabaha kuu ya utaratibu wa udhamini kwa mujibu wa madhumuni ya Umoja wa Mataifa yaliyomo katika Ibara ya kwanza (1) ya Mkataba huu, yatakuwa ni:

a. Kuendeleza amani na usalama wa kimataifa;
b. Kukuza maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii, na kielimu ya wakazi wa nchi zilizo chini ya udhamini, na kuwaendeleza katika kujipatia serikali ya madaraka au uhuru pale itakapoonekana inafaa kutegemeana na mazingira ya kila nchi na watu wake na kutekeleza matakwa ya wananchi husika kulingana na masharti ya Mikataba ya udhamini;

c. Kuhimiza haki za binadamu na uhuru wa msingi kwa wote bila ubaguzi kwa misingi ya taifa, jinsia, lugha au dini na kuhimiza kutambuliwa kwa uhuru wa wote duniani; na

d. Kuhakikisha haki zinatendeka katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kibiashara kwa nchi Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa na watu wake na pia kutendewa haki watu katika utawala wa haki chini ya sheria bila upendeleo katika kufanikisha shabaha na masharti ya ibara ya 80.

## Ibara ya 77

1. Utaratibu wa Udhamini utatumiwa kwa nchi zilizo katika makundi yafuatayo kulingana na Mikataba ya udhamini:
   a. Nchi ambazo zipo chini ya uangalizi wa utawala maalumu.
   b. Nchi ambazo zimejitenga na mataifa adui kutokana na matokeo ya vita vya pili vya dunia.
   c. Nchi ambazo kwa hiari yao wenyewe zimejiweka chini ya utawala wa mataifa mengine.

2. Itategemea Mikataba kwa nchi katika makundi hayo kuwekwa katika utaratibu wa udhamini na kwa masharti gani.

## Ibara ya 78

Utaratibu wa udhamini hautatumika kwa nchi ambazo zimekuwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa, ambapo uhusiano miongoni mwa nchi hizo utazingatia kuheshimu uhuru na utaifa wa kila nchi.

## Ibara ya 79

Masharti ya udhamini, kwa kila nchi iliyo chini ya taratibu za udhamini, ikiwa ni pamoja na mabadiliko au marekebisho, yatakubaliwa na mataifa husika yakiwemo mataifa tawala kwa nchi ambazo ziko chini ya utawala maalum wa Mwanachama wa Umoja wa Mataifa na masharti hayo yatathibitishwa na mujbu wa masharti katika Ibara za 83 na 85.

## Ibara ya 80

1. Isipokuwa kama itakavyokubalika katika kila Mikataba ya udhamini ambayo imetajwa katika Ibara za 77, 79 na 81, zinazoweka kila nchi chini ya utaratibu wa udhamini na mpaka Mikataba hiyo itapokubaliwa, hakuna kilichopo ndani ya Sura hii kitakachoweza kubadilisha kwa namna yeyote ile haki za mataifa au watu au masharti ya makubaliano ya kimataifa ambayo yanahusisha Wanachama wa Umoja wa Mataifa.
2. Aya ya kwanza (1) ya Ibara hii haitatafsiriwa kama inatoa mwanya wa kuchelewesha au

kuahirisha mazungumzo na mapatano ya Mikataba ya kuweka nchi chini ya utaratibu wa udhamini kama inavyoelezwa katika Ibara ya 77.

## Ibara ya 81

Kila Mkataba wa udhamini utajumuisha masharti ambayo nchi iliyodhaminiwa itatawaliwa na kuchagua utawala utakaoiongoza nchi hiyo. Utawala kama huo, utaitwa 'uongozi tawala' na unaweza ukawa ni taifa moja au zaidi au Umoja wa Mataifa wenyewe.

## Ibara ya 82

Kunaweza kuwepo katika Mkataba wowote wa udhamini, eneo au maeneo maalum ambayo yanaweza kujumuishwa katika nchi ya udhamini bila upendeleo katika Mkataba au Mikataba yoyote iliyotajwa katika Ibara ya 43.

## Ibara ya 83

1. Kazi zote za Umoja wa Mataifa zinazohusiana na maeneo maalumu zikiwemo za kupitisha masharti ya Mikataba ya udhamini pamoja na kubadilishwa au kurekebishwa kwake, zitafanywa na Baraza la Usalama.
2. Lengo kuu lililoelezwa katika Ibara ya 76 litahusu watu waliopo katika maeneo maalumu.
3. Baraza la Usalama, kulingana na masharti yaliyomo katika Mikataba ya udhamini na bila

upendeleo kwa masuala ya kiulinzi, litatoa msaada kwa Baraza la Udhamini ili kutimiza majukumu ya Umoja wa Mataifa chini ya utaratibu wa udhamini katika nyanja za kisiasa, kichumi, kijamii na kielimu katika maeneo hayo maalumu.

## Ibara ya 84

Itakuwa ni kazi ya nchi tawala kuhakikisha kwamba nchi iliyodhaminiwa inajishughulisha katika kudumisha amani na usalama wa kimataifa. Hivyo, kila nchi tawala inaweza kutumia majeshi, huduma na msaada kutoka nchi iliyodhaminiwa ili kutimiza majukumu ya Baraza la Usalama ambayo yanatekelezwa kwa niaba na nchi tawala na kudumisha usalama na utawala wa sheria katika nchi iliyodhaminiwa.

## Ibara ya 85

1. Kazi za Umoja wa Mataifa kuhusu Mikataba ya udhamini katika maeneo yote ambayo siyo maalumu, ikiwa ni pamoja na kuidhinisha masharti ya Mikataba ya udhamini, kuibadilisha au kuirekebisha, zitafanywa na Baraza Kuu.
2. Baraza la Udhamini likifanya kazi chini ya uongozi wa Baraza Kuu litalisaidia Baraza kuu katika utendaji wa kazi zake.

# SURA YA XIII

# BARAZA LA UDHAMINI

## Muundo

### Ibara ya 86

1. Baraza la Udhamini linaundwa na Wanachama wafuatao wa Umoja wa Mataifa:
   a. Wanachama wote wanaotawala nchi zilizo chini ya udhamini;
   b. Wanachama wote waliotajwa kwa majina katika Ibara ya 23 ambao hawatawali nchi zilizo chini ya udhamini.
   c. Wanachama wote waliochaguliwa kwa kipindi cha miaka mitatu na Baraza Kuu kama itahitajika kuhakikisha kwamba idadi ya Wanachama wa Baraza la Udhamini inagawanywa sawa kati ya Wanachama wa Umoja wa Mataifa wanaotawala nchi zilizo chini ya udhamini na Wanachama ambao hawatawali nchi zilizo chini ya udhamini.
2. Kila Mwanachama wa Baraza la Udhamini atachagua mtu mmoja mwenye sifa zinazotakiwa kumwakilisha.

## Kazi na Mamlaka

### Ibara ya 87

Baraza la Udhamini, chini ya mamlaka ya Baraza Kuu, litafanya kazi zifuatazo:

a. Litaangalia taarifa zilizowasilishwa na nchi tawala;
b. Litakubali maombi na kuyachunguza kwa kushauriana na nchi tawala;
c. Litapanga ratiba ya kuzitembelea nchi zilizo chini ya udhamini wake katika muda uliokubaliwa na nchi tawala; na
d. Kutimiza kazi hizi na nyinginezo kulingana na masharti yaliyomo katika Mikataba ya udhamini.

### Ibara ya 88

Baraza la Udhamini litatayarisha dodoso - orodha ya maswali - juu ya maendeleo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kielimu ya wakazi waliomo katika kila nchi iliyo chini ya udhamini na nchi inayotawala kwa niaba ya Baraza Kuu na kutoa taarifa ya mwaka kwa Baraza Kuu juu ya masuala hayo.

## Upigaji kura

### Ibara ya 89

1. Kila Mwanachama wa Baraza la Udhamini atakuwa na kura moja katika baraza hilo.

2. Maamuzi ya Baraza la Udhamini yatafikiwa na wingi wa Wanachama waliopo na watakaopiga kura.

## Taratibu

### Ibara ya 90

1. Baraza la Udhamini litafuata kanuni na sheria zake ukiwemo utaratibu za kumchagua raisi wake.
2. Baraza la Udhamini litakutana kama inavyotakiwa kulingana na kanuni zake ambazo zinajumuisha masharti ya kuitisha mikutano baada ya kuombwa na Wanachama walio wengi.

### Ibara ya 91

Baraza la Udhamini, pale inapohitajika litajitolea kulisaidia Baraza la Uchumi na Jamii na mashirika maalum katika masuala yanayohusu mabaraza hayo.

## SURA YA XIV

# MAHAKAMA YA KIMATAIFA

### Ibara ya 92

Mahakamaya Kimataifa itakuwa ni chombo kikuu cha haki cha Umoja wa Mataifa. Itafanya kazi kulingana na sheria zilizoambatanishwa ambazo zimo katika sheria za Mahakamaya kudumu ya kimataifa na ni sehemu muhimu ya Mkataba huu.

### Ibara ya 93

1. Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ni sehemu ya "ipso facto" ya sheria za Mahakama ya Kimataifa.
2. Nchi ambayo si Mwanachama wa Umoja wa Mataifa inaweza kuwa sehemu ya sheria za Mahakama ya Kimataifa kwa masharti yatakayoamuliwa na Baraza kuu baada ya kupendekezwa na Baraza la Usalama.

### Ibara ya 94

1. Kila Mwanachama wa Umoja wa Mataifa anatakiwa kukubaliana na maamuzi ya Mahakamaya Kimataifa katika kila shauri linalomhusu.
2. Kama upande ulio na shauri utashindwa kutimiza maamuzi yaliyotolewa na mahakama, upande

mwingine unaweza kuomba msaada kwenye Baraza la Usalama kama itakuwa lazima ambalo litatoa mapendekezo au kuamua ,juu ya hatua zitakazochukuliwa ili kutekeleza maamuzi ya mahakama.

## Ibara ya 95

Hakuna kipengele ndani ya Mkataba huu kinachowazuia Wanachama wa Umoja wa Mataifa kupeleka maamuzi kuhusu malalamiko yao kwenye Mabaraza mengine ya sheria kutokana na Mikataba iliyopo au Mikataba itakayokubaliwa baadaye.

## Ibara ya 96

1. Baraza Kuu au Baraza la Usalama linaweza kutoa ushauri juu ya suala lolote la kisheria.
2. Vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa na mashirika maalum, ambayo katika muda wowote yanaweza kupewa mamlaka na Baraza kuu, yanaweza kuomba ushauri wa Mahakama juu ya masuala ya kisheria yanayojitokeza katika shughuli zake.

## SURA YA XV

# SEKRETARIETI

### Ibara ya 97

Sekretarieti itajumuisha Katibu Mkuu na wafanyakazi wengine kama Umoja utakavyohitaji. Katibu Mkuu atachaguliwa na Baraza Kuu baada ya mapendekezo ya Baraza la Usalama. Atakuwa Afisa Utawala mkuu wa Umoja wa Mataifa.

### Ibara ya 98

Katibu Mkuu atafanya kazi katika wadhifa huo katika mikutano yote ya Baraza Kuu, Baraza la Usalama, Baraza la Uchumi na Jamii na Baraza la Udhamini na atafanya kazi nyingine atazokabidhiwa na vyombo hivyo. Katibu Mkuu atatoa taarifa ya mwaka kwa Baraza Kuu juu ya kazi za Umoja wa Mataifa.

### Ibara ya 99

Katibu Mkuu anaweza kuliarifu Baraza la Usalama suala lolote ambalo kwa maoni yake anaona linaweza kutishia udumishwaji wa amani na usalama wa kimataifa.

### Ibara ya 100

1. Katika utendaji wa kazi zao, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote hawatakiwi kuomba au

kupokea maelekezo kutoka serikali au mamlaka yoyote nje ya Umoja wa Mataifa. Watajizuia kushiriki katika vitendo vyovyote vinavyoweza kuwayumbisha kama Maafisa wa Umoja wa Mataifa.

2. Kila Mwanachama wa Umoja wa Mataifa anatakiwa kuheshimu hadhi ya kimataifa na kazi za Katibu Mkuu na wafanyakazi wa Umoja wa Mataifa bila kuwarubuni katika utendaji wao wa kazi.

## Ibara ya 101

1. Wafanyakazi watachaguliwa na Katibu Mkuu chini ya taratibu zilizowekwa na Baraza Kuu.
2. Wafanyakazi wanaofaa watapewa kazi za kudumu katika Baraza la Uchumi na Jamii, Baraza la Udhamini na kama inatakiwa katika vyombo vingine vya Umoja wa Mataifa. Wafanyakazi hao watakuwa ni sehemu ya Sekretarieti.
3. Uangalizi mkubwa katika kuajiri wafanyakazi na kuweka hali nzuri ya kazi utakuwa ni muhimu katika kuhakikisha hali nzuri ya utendaji kazi, ufanisi, tija na uaminifu vinakuwepo. Umuhimu unaostahili utatolewa pale inapowezekana kuajiri wafanyakazi sehemu waliko.

# SURA YA XVI
# MASHARTI MBALI MBALI

## Ibara ya 102

1. Kila Mkataba na Makubaliano ya kimataifa yanayofanywa na kila Mwanachama wa Umoja wa Mataifa baada ya Mkataba uliopo kuanza kutumika yatatakiwa kusajiliwa mapema iwezekanavyo na Sekretarieti na kuchapishwa.
2. Hakuna mwanachama yeyote ambaye ni sehemu ya Mkataba au makubaliano ya kimataifa ambayo hayajasajiliwa kulingana na masharti yaliyopo katika aya ya kwanza (1) ya Ibara hii anaweza kuyatumia kwa chombo chochote cha Umoja wa Mataifa.

## Ibara ya 103

Wakati wa mgogoro kati ya majukumu ya Wanachama wa Umoja wa Mataifa chini ya Mkataba wa sasa na majukumu yao chini ya Mikataba mingine yoyote ya kimataifa, wajibu wao chini ya Mkataba huu utaendelea.

## Ibara ya 104

Umoja wa Mataifa utanufaika kama kila nchi ambayo ni Mwanachama itatekeleza kazi za Umoja huo na majukumu yake na kufanikisha madhumuni yake.

**Ibara ya 105**

1. Umoja utanufaika kama kila nchi ambayo ni Mwanachama wake itakuwa na haki na itapata faida katika utekelezaji wa majukumu na kufanikisha madhumuni ya Umoja huo.
2. Wawakilishi wa Wanachama wa Umoja wa Mataifa na Maofisa wa Umoja huo hali kadhalika kwa pamoja watanufaika na haki na faida hizo kama watafanya kazi zao wakiwa huru.
3. Mkutano mkuu wa Umoja wa Mataifa unaweza kutoa mapendekezo yake kuhusu namna ya kutumia masharti katika aya ya kwanza (1) na ya pili (2) ya Ibara hii au unaweza kupendekeza mikataba kwa Wanachama wa Umoja huo kwa madhumuni hayo.

## SURA YA XVII

# MIPANGO YA MPITO YA USALAMA

### Ibara ya 106

Kabla ya utekelezaji wa makubaliano maalumu yanayoelezwa katika Ibara ya 43 na kama Baraza la Usalama litapenda, yanaliwezesha Baraza hilo kuanza majukumu yake yaliyomo katika Ibara ya 42. Nchi nne zilizotia saini Tamko la Moscow la tarehe 30 Oktoba 1943 na Ufaransa kwa mujibu wa masharti yaliyo katika aya ya tano (5) ya Tamko hilo, zitashauriana kulingana na hali itakavyokuwa na wanachama wengine wa Umoja wa Mataifa kwa madhumuni ya kuchukua hatua za pamoja kwa niaba ya Umoja wa Mataifa kama italazimu kwa lengo la kudumisha amani na usalama wa kimataifa.

### Ibara ya 107

Hakuna kipengele ndani ya Mkataba wa sasa kitakacho tengua au kuzuia hatua itakayochukuliwa kwa nchi yoyote ambayo wakati wa Vita vikuu vya Pili vya dunia imekuwa ni adui wa nchi yoyote iliyotia saini Mkataba wa sasa kutokana na vita hivyo.

## SURA YA XVIII

# MAREKEBISHO

### Ibara ya 108

Marekebisho ya Mkataba wa sasa yataanza kutumika wakati Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa wameyakubali kwa theluthi mbili ya kura za wanachama wote wa Baraza Kuu na kuridhiwa kulingana na taratibu za kikatiba za theluthi mbili za Wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ikiwa ni pamoja na Wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama.

### Ibara ya 109

1. Mkutano Mkuu wa Wanachama wa Umoja wa Mataifa wa kupitia Mkataba wa sasa unaweza kufanyika tarehe na mahali patakapopangwa na theluthi mbili ya kura za Wanachama wote wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa na kura ya Mwanachama yeyote kati ya Wanachama tisa wa Baraza la Usalama. Kila Mwanachama wa Umoja wa Mataifa atakuwa na kura moja katika mkutano huo.
2. Badiliko lolote ndani ya Mkataba huu lililopendekezwa kwa theluthi mbili ya kura zilizopigwa katika mkutano mkuu huo litaanza

kutumika pale litakaporidhiwa kulingana na taratibu za kikatiba za theluthi mbili ya wanachama wote wa Umoja wa Mataifa ikiwa ni pamoja na Wanachama wote wa kudumu wa Baraza la Usalama.

3. Endapo mkutano huo haukufanyika kabla ya kikao cha kumi cha mwaka cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa baada ya Mkataba wa sasa kuanza kutumika, pendekezo la kuitisha mkutano wa namna hiyo litawekwa kwenye agenda ya kikao hicho cha Baraza Kuu na mkutano huo utafanyika kama itaamuliwa kufanya hivyo na kura nyingi za Wanachama wa Baraza Kuu na kwa kura ya Mwanachama yeyote kati ya Wanachama saba wa Baraza la Usalama.

## SURA YA XIX

# KURIDHIA NA KUTIA SAINI

**Ibara ya 110**

1. Mkataba wa sasa utaridhiwa na nchi zilizotia saini kulingana na taratibu zao za kikatiba.
2. Kuridhia huko kutawekwa chini ya serikali ya Marekani, ambayo itazifahamisha nchi zote zilizotia saini Mkataba huo pamoja na Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa pindi anapoteuliwa.
3. Mkataba wa sasa ili uanze kutumika utategemea ridhaa ya Jamhuri ya watu wa China, Ufaransa, Urusi, Uingereza, Ireland ya kaskazini, na Marekani pamoja na nchi nyingi zilizotia saini Mkataba huo. Protokali ya maridhio yaliyofanywa na kuwekwa chini ya Serikali ya Marekani yatafanywa na serikali hiyo ambayo itatawanya nakala za Mkataba kwa nchi zote zilizotia saini.
4. Nchi zilizotia saini Mkataba huo na ambazo zimeuridhia baada ya kuanza kutumika ndizo zitakuwa Wanachama waanzilishi wa Umoja wa Mataifa tangu tarehe ziliporidhia Mkataba huo.

## Ibara ya 111

Mkataba huu wa sasa ambao umo katika lugha ya kichina, kifaransa, kirusi, kiingereza na kihispania ni Mkataba halisi kama Mikataba mingine na utaendelea kuwekwa katika Jumba la Mambo ya kale la serikali ya Marekani. Nakala zilizothibitishwa zitasambazwa na Marekani kwa serikali zilizotia saini Mkataba huo.

Kwa imani, wawakilishi wa serikali katika Umoja wa Mataifa wametia saini Mkataba wa sasa.

Kitendo kilichofanyika katika mji wa San Fransisko siku ya tarehe ishirini na sita ya Juni, elfu moja mia tisa na arobaini na tano.

# SHERIA YA MAHAKAMA YA KIMATAIFA

## Ibara ya 1

Mahakama ya Kimataifa inayoanzishwa na Mkataba wa Umoja wa Mataifa kama chombo kikuu cha haki cha Umoja wa Mataifa itaundwa na kufanya kazi kulingana na masharti ya sheria ya sasa.

## SURA YA I

# UTARATIBU WA KAZI WA MAHAKAMA

### Ibara ya 2

Mahakama itaundwa na bodi ya majaji huru, waliochaguliwa bila kufuata utaifa wao kutoka miongoni mwa watu wenye tabia adilifu ya hali ya juu ambao wana sifa zinazohitajika ndani ya nchi zao zenye kuwawezesha kuteuliwa katika ngazi za juu za Mahakama au wana sifa za kutoa ushauri wa kimahakama katika sheria za kimataifa.

### Ibara ya 3

1. Mahakama itajumuisha Wanachama 15 na kusiwepo Wanachama wawili wanaowakilisha Taifa moja.
2. Mtu ambaye, kwa madhumuni ya uanachama wake katika Mahakama, ataonekana ni mwananchi wa zaidi ya taifa moja, atahesabiwa kama mwananchi wa taifa ambako ana haki zote za kiraia na kisiasa.

### Ibara ya 4

1. Wanachama wa Mahakama ya Kimataifa watachaguliwa na Baraza Kuu na Baraza la Usalama kutoka katika orodha ya watu

watakaoteuliwa na vikundi vya kitaifa katika Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi, kulingana na masharti yafuatayo.

2. Kwa Wanachama wa Umoja wa Mataifa, ambayo hayana uwakilishi wa kudumu katika Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi, watateuliwa na vikundi vya kitaifa vilivyochaguliwa kwa madhumuni hayo na serikali zao chini ya masharti ambayo yameelezwa kwa Wanachama wa Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi katika Ibara ya 44 ya Mkataba wa mwaka 1907 wa The Hague wa kutatua migogoro ya kimataifa.
3. Masharti ya taifa linalohusika na Sheria za sasa za Mahakama ya Kimataifa lakini siyo Mwanachama wa Umoja wa Mataifa, kuweza kushiriki katika kuchagua Wanachama wa Mahakama, kama hakuna Mkataba maalumu, yatawekwa na Baraza Kuu baada ya kupendekezwa na Baraza la Usalama.

## Ibara ya 5

1. Angalau miezi mitatu kabla ya tarehe ya uchaguzi, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa atawapelekea ombi la kimaandishi Wanachama wa Mahakama ya Kudumu ya Usuluhishi wa nchi ambazo zinahusika na Sheria ya sasa na kwa

Wanachama wa vikundi vya kitaifa waliochaguliwa chini Ibara ya 4 aya ya pili (2), la kuwakaribisha kuteua watu watakaokabidhiwa kazi za mahakama katika kipindi watakachopewa.

2. Hakuna kikundi ambacho kinaweza kuteua watu zaidi ya wanne, wawili kati yao kutoka taifa moja. Idadi ya watakaoteuliwa hairuhusiwi kuzidi mara mbili ya nafasi zinazohitajika kujazwa.

## Ibara ya 6

Kabla ya kuteua majina ya watu, kila kikundi cha kitaifa, inapendekezwa, kishauriane na chombo chake cha juu cha Mahakama, taasisi zake za kisheria, vyuo vyake vya kisheria na wasomi wake wa sheria.

## Ibara ya 7

1. Katibu Mkuu atatayarisha orodha ya watu walioteuliwa kwa kufuata herufi za Alphabeti. Kama ilivyotajwa katika Ibara ya 12, aya ya pili (2), hawa ndiyo wanafaa.
2. Katibu Mkuu atawasilisha orodha hiyo kwa Baraza Kuu na kwa Baraza la Usalama.

## Ibara ya 8

Baraza Kuu na Baraza la Usalama vitaendelea bila kutegemeana kuchagua Wanachama wa Mahakama.

## Ibara ya 9

Katika kila uchaguzi, wachaguaji lazima wakumbuke kuwa watu watakaochaguliwa siyo tu wana sifa zinazohitajika lakini vile vile uwakilishi wao katika chombo hicho lazima uwe wa kistaarabu na unaofuata misingi ya sheria duniani.

## Ibara ya 10

1. Watu watakaopata kura nyingi katika Baraza Kuu na Baraza la Usalama watahesabiwa kuwa wamechaguliwa.
2. Kura yeyote ya Baraza la Usalama, iwe ya uchaguzi wa majaji au ya uteuzi wa Wanachama wa mkutano unaotajwa kama Ibara ya 12, itachukuliwa bila kutofautisha Wanachama wa kudumu au wanachama wasio wa kudumu wa Baraza la Usalama.
3. Katika tukio ambapo mwananchi zaidi ya mmoja kutoka taifa moja wanapata kura nyingi katika Baraza Kuu na Baraza la Usalama, mwenye umri mkubwa kati yao atahesabiwa kuwa kachaguliwa.

## Ibara ya 11

Kama baada ya mkutano wa mwanzo wa uchaguzi, nafasi moja au zaidi zikabakia bila kujazwa, mkutano wa pili au hata ikilazimu wa tatu unaweza ukafanywa.

**Ibara ya 12**

1. Kama baada ya mkutano wa tatu, nafasi moja au zaidi zitabaki bila kujazwa, mkutano wa pamoja utakaojumuisha Wanachama sita, watatu waliochaguliwa na Baraza Kuu na watatu Baraza la Usalama, utaitishwa wakati wowote kwa ombi la Baraza Kuu au Baraza la Usalama kwa madhumuni ya kuchagua kwa kupiga kura jina moja kwa kila nafasi iliyo wazi na kuwasilisha kwa Baraza Kuu na Baraza la Usalama ili vyombo hivyo viyakubali.
2. Kama mkutano huo wa pamoja kwa kauli moja utapata jina la mtu mwenye sifa zote zinazohitajika, anaweza kuingizwa katika orodha itakayopitishwa na mkutano huo hata kama hakuwekwa katika orodha ya watu walioteuliwa kama inavyoelezwa katika Ibara ya 7.
3. Kama mkutano huo wa pamoja utaridhika kwamba hautafanikiwa katika kufanikisha uchaguzi huo, Wanachama wa Mahakama ambao tayari wamekwisha chaguliwa wataendelea kujaza nafasi zilizo wazi kwa kuchaguliwa katika muda ambao utawekwa na Baraza la Usalama kutoka miongoni mwa Wanachama ambao wamepata kura kutoka Baraza Kuu au Baraza la Usalama .

4. Katika tukio ambapo kutakuwa na kura sawa zilizopigwa na majaji, Jaji mwenye umri mkubwa atakuwa na kauli ya mwisho ya kura.

## Ibara ya 13

1. Wanachama wa Mahakama watachaguliwa kwa kipindi cha miaka tisa na wanaweza kuchaguliwa tena ikiwa kati ya majaji waliochaguliwa katika uchaguzi wa kwanza, kipindi cha majaji watano kitakwisha baada ya miaka mitatu na kipindi cha majaji watano zaidi kitakwisha baada ya miaka sita.
2. Majaji ambao vipindi vyao vya kazi vinaisha mwishoni mwa miaka iliyotajwa hapo juu, watachaguliwa kutoka katika orodha itakayotolewa na Katibu Mkuu mara baada ya uchaguzi wa kwanza kumalizika.
3. Wanachama wa Mahakama wataendelea kufanya kazi zao mpaka pale nafasi zao zitakapojazwa. Hata kama zitajazwa, majaji hao wataendelea kumaliza mashauri yao waliyokuwa wamekwisha yaanza.
4. Katika suala la kujiuzulu Mwanachama wa Mahakama, kujiuzulu huko kutawasilishwa kwa Rais wa Mahakama ambaye atapeleka kwa Katibu Mkuu. Kitendo hicho cha mwisho kinaifanya nafasi hiyo iwe wazi.

**Ibara ya 14**

Nafasi zote zitajazwa kwa utaratibu kama ule uliofanywa katika uchaguzi wa kwanza, kwa masharti yafuatayo: Katibu Mkuu katika kipindi cha mwezi mmoja tangu nafasi itokee atatoa tangazo kama Ibara ya 5 inavyoeleza na tarehe ya uchaguzi itapangwa na Baraza la Usalama.

**Ibara ya 15**

Mwanachama wa Mahakama aliyechaguliwa kujaza nafasi ya mwanachama ambaye muda wake ulikuwa bado haujamalizika, ataishikilia ofisi kwa kipindi chote kilichobakia cha Mwanachama aliyemtangulia.

**Ibara ya 16**

1. Hakuna Mwanachama wa Mahakama ambaye atafanya kazi za kisiasa au za utawala au kujihusisha na kazi nyingine nje ya kazi za Mahakama.
2. Wasiwasi wowote juu ya kifungu hicho utatafutiwa ufumbuzi na uamuzi na Mahakama.

**Ibara ya 17**

1. Hakuna Mwanachama wa Mahakama ambaye atafanya kazi kama wakala, mshauri au wakili katika kesi yoyote ile.
2. Hakuna Mwanachama ambaye atashiriki kutoa maamuzi katika kesi yoyote ambayo tayari alikwishawahi kushiriki kama wakala, mshauri

au wakili kwa upande mmojawapo au kama mjumbe wa Mahakama ya kitaifa au ya kimataifa au tume ya uchunguzi au katika nafasi yoyote ile.

3. Wasiwasi wowote utakaojitokeza kuhusu kifungu hicho utatafutiwa ufumbuzi na uamuzi na Mahakama.

**Ibara ya 18**

1. Hakuna Mwanachama wa Mahakama ambaye atafukuzwa mpaka Wanachama wengine wamefikia uamuzi kwamba ameshindwa kutimiza wajibu wake.
2. Taarifa rasmi lazima itolewe kwa Katibu Mkuu na Msajili wa Mahakama juu ya uamuzi huo.
3. Taarifa hiyo itaifanya nafasi hiyo kuwa wazi.

**Ibara ya 19**

Wanachama wa Mahakama, wakiwa katika masuala ya kimahakama, watakuwa na haki na faida za kibalozi.

**Ibara ya 20**

Kila Mwanachama wa Mahakama, kabla ya kuanza kutekeleza majukumu yake atakula kiapo mbele ya Mahakama kuwa atatumia madaraka yake bila upendeleo na kwa umakini.

## Ibara ya 21

1. Mahakama itachagua Rais na Makamu wa Rais kwa kipindi cha miaka mitatu na wanaweza kuchaguliwa tena.
2. Mahakama itamteua Msajili wake na inaweza kuwateua maofisa wengine kama itakuwa lazima.

## Ibara ya 22

1. Makao makuu ya Mahakama yatakuwa The Hague. Hii haimaanishi kwamba Mahakama haiwezi kuwa na vikao na kufanya shughuli zake mahali pengine inapoona panafaa.
2. Rais na Msajili wa Mahakama, watakuwa na makao yao mahali ambapo Makao makuu ya Mahakama yapo.

## Ibara ya 23

1. Mahakama itaendelea kufanya vikao vyake vya kawaida vya kusikiliza kesi moja kwa moja isipokuwa wakati wa likizo ambazo tarehe na muda wake zitapangwa na Mahakama.
2. Wanachama wa Mahakama watakuwa na haki ya kuwa na likizo za mara kwa mara ambazo tarehe na muda wake vitapangwa na Mahakama baada ya kuzingatia umbali wa kutoka The Hague na mahali ambapo kila Jaji anatoka.

3. Wanachama wa Mahakama watatakiwa kufanya kazi za Mahakama isipokuwa pale ambapo wako likizo, wanaumwa au wana sababu nyingine muhimu watakazozitoa kwa Rais wa Mahakama.

## Ibara ya 24

1. Kama kwa sababu maalumu, Mwanachama wa Mahakama ataona ni vema asishiriki katika maamuzi ya kesi fulani, anatakiwa kumweleza Rais wa Mahakama.
2. Kama Rais ataona kwa sababu maalumu kuwa Mwanachama mmoja wa Mahakama asishiriki kwenye kikao fulani, lazima amtaarifu.
3. Kama katika kesi yoyote Mwanachama wa Mahakama na Rais hawakubaliani, tatizo hilo lifikiwe ufumbuzi kwa uamuzi wa Mahakama.

## Ibara ya 25

1. Mahakama itaendesha vikao vyake kamili isipokuwa pale ambapo imeelezwa vinginevyo katika sheria za Mahakama.
2. Kutegemeana na masharti kwamba idadi ya majaji watakaopatikana kuunda Mahakama isipungue chini ya kumi na moja, sheria za Mahakama zinaweza kuruhusu Jaji mmoja au zaidi kutegemeana na mazingira na mzunguko, kutohudhuria vikao vya Mahakama.

3. Idadi ya chini kabisa ya majaji tisa inatosha kuendesha vikao vya Mahakama

**Ibara ya 26**

1. Mahakama mara kwa mara inaweza kuwa na chemba moja au zaidi ya itakayojumuisha majaji watatu au zaidi kulingana na maamuzi ya Mahakama, kushughulikia aina fulani ya kesi kwa mfano kesi za kazi au kesi zinazohusiana na mawasiliano na uchukuzi.
2. Mahakama wakati wowote inaweza kuwa na chemba itakayoshughulikia kesi ya aina fulani. Idadi ya majaji watakaokuwa katika chemba hiyo itaamuliwa na Mahakama baada ya kukubaliwa na pande zote zinazohusika na kesi hiyo.
3. Kesi zitasikilizwa na kuamuliwa na chemba zilizotajwa katika Ibara hii kama pande husika zitaomba iwe hivyo.

**Ibara ya 27**

Hukumu itakayotolewa na chemba yoyote kati ya zilizotajwa katika Ibara za 26 na 29 zitachukuliwa kama ni maamuzi ya Mahakama.

**Ibara ya 28**

Chemba zinazotajwa katika Ibara za 26 na 29 zinaweza kwa idhini ya pande husika kukaa na kutenda kazi zake mahala pengine zaidi ya makao makuu ya The Hague.

**Ibara ya 29**

Kwa madhumuni ya kuharakisha kazi za Mahakama, Mahakama itaunda kila mwaka chemba yenye majaji watano ambayo kwa ombi la pande zinazohusika inaweza kusikiliza na kuamua kesi kwa taratibu fupi. Kwa nyongeza, majaji wawili watachaguliwa kwa madhumuni ya kuwabadilisha majaji ambao wataona hawawezi kukaa katika kikao.

**Ibara ya 30**

1. Mahakama itaweka sheria za kuendesha shughuli zake. Kwa ujumla itaunda sheria zake na kanuni.
2. Sheria ya Mahakama inaweza kuruhusu wazee wa baraza kuhudhuria vikao vya Mahakama au vikao vya chemba bila yakuwa na haki ya kupiga kura.

**Ibara ya 31**

1. Majaji wa mataifa ambayo yanahusika katika kesi wanayo haki ya kuhudhuria kikao cha kesi katika Mahakama.
2. Kama Baraza la Mahakama litakuwa na Jaj ambaye ni mwananchi wa taifa ambalo linahusik na kesi hiyo, upande mwingine wowote unawez kumchagua mtu kukaa kama Jaji. Mtu huy atachaguliwa kutoka katika orodha ya wat

walioteuliwa kama wajumbe kulingana na masharti katika Ibara za 4 na 5. 3 .
Kama Mahakama itakuwa na Baraza ambalo halina Jaji ambaye ni mwananchi wa taifa ambalo linahusika na kesi, kila upande unaweza kuchagua Jaji kulingana na masharti katika aya ya pili (2) ya Ibara hii.

4. Masharti ya Ibara hii yatatumika katika kesi zilizotajwa katika Ibara za 26 na 29. Katika kesi kama hizo, Rais wa Mahakama atamuomba Mjumbe mmoja au kama italazimu wawili wa Mahakama wanaounda chemba kuwapisha Wanachama wa Mahakama ambao ni wananchi wa mataifa yanayohusika na kesi hiyo, na ikishindikana au kama hawatakuwepo, majaji watakaochaguliwa na pande zinazohusika watashika nafasi hizo.
5. Kama kuna pande nyingi zinazohusika na kesi hiyo, pande hizo kwa madhumuni ya masharti ya kuendesha kesi, zitachukuliwa kama upande mmoja tu. Utata wowote kuhusu suala hilo utatatuliwa na maamuzi ya Mahakama.
6. Majaji watakaochaguliwa kama ilivyoelezwa katika aya za pili (2), tatu (3) na nne (4) za Ibara hii watatimiza masharti yanayotakiwa katika

Ibara za 2, 17(aya ya pili), 20 na 24 ya sheria za sasa za Mahakama. Watashiriki kutoa uamuzi kwa misingi ya usawa kama wenzao.

**Ibara ya 32**

1. Kila Mjumbe wa Mahakama atapata mshahara wake wa mwaka.
2. Rais atapata masurufu maalumu ya mwaka.
3. Makamu wa Rais atapata masurufu maalumu kwa kila siku anapofanya kazi kama Rais.
4. Majaji waliochaguliwa chini ya Ibara ya 31, ambao siyo Wanachama wa Mahakama, watalipwa fidia kwa kila siku ambapo watakuwa kazini.
5. Viwango vya mishahara, masurufu na fidia hizo vitawekwa na Baraza Kuu. Viwango hivyo haviwezi vikapunguzwa wakati wa kipindi chao cha kazi.
6. Kiwango cha mshahara wa Msajili kitawekwa na Baraza Kuu kutokana na pendekezo la Mahakama.
7. Kanuni zilizowekwa na Baraza Kuu zitaweka masharti ya malipo ya pensheni ya Wanachama na Msajili wa Mahakama baada ya kustaafu, na masharti yanayoelezea jinsi ya kurejeshewa gharama za usafiri kwa Wanachama wa

Mahakama na Msajili.

8. Mishahara, masurufu na fidia zilizotajwa hapo juu hazitatozwa kodi.

## Ibara ya 33

Gharama za Mahakama zitafidiwa na Umoja wa Mataifa kama itakavyo amuliwa na Baraza Kuu.

# SURA YA II

# UWEZO WA MAHAKAMA

## Ibara ya 34

1. Ni nchi tu ambazo zinaweza kuhusika na kesi zinazopelekwa Mahakamani.
2. Mahakama, kulingana na kufuatana na sheria zake, inaweza kuomba maelezo kutoka mashirika ya kimataifa yanayohusika na kesi zilizopo mbele ya Mahakama na itapokea maelezo hayo yatakayotolewa na mashirika hayo kwa juhudi za mashirika yenyewe.
3. Pale ambapo mashirika ya kimataifa yaliyoshirikishwa katika kufikia makubaliano ambayo yameleta utata na utata huo ukafikishwa mbele ya Mahakama, Msajili wa Mahakama atawasiliana na mashirika hayo na atayapatia nakala za uendeeshaji wa kesi hiyo Mahakamani.

## Ibara ya 35

1. Mahakama itashirikisha mataifa yote ambayo yamekubaliana na sheria za sasa.
2. Masharti ambayo yataifanya Mahakama kushirikisha mataifa mengine kulingana na makubaliano yanayohusu Mikataba iliyopo, yatatolewa na Baraza la Usalama lakini hakuna

masharti yoyote yatakayozinyima pande zote haki sawa mbele ya Mahakama.

3. Pale itakapotokea taifa ambalo siyo Mwanachama wa Umoja wa Mataifa linahusika na kesi, Mahakama itaweka kiwango cha gharama kitakachotolewa na taifa hilo kugharamia shughuli za Mahakama katika kesi hiyo. Masharti hayo hayatatumika kama taifa hilo limo katika mataifa yanayochangia kulipa gharama za Mahakama hiyo.

## Ibara ya 36

1. Mahakama itakuwa na mamlaka juu ya kesi zote ambazo mataifa yanahusika nazo na mambo yote ambayo yametajwa katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa au yametajwa katika Mikataba mbali mbali inayotumika.
2. Mataifa ambayo yanakubaliana na sheria za Mahakama yanaweza wakati wowote kutangaza, 'ipso facto' ni ya lazima bila kuhitaji makubaliano maalumu, na taifa jingine lolote ambalo linaamini hivyo, kuwa Mahakama ina mamlaka katika mambo yote ya migogoro ya kisheria inayohusu:
   a. kufafanuliwa kwa Mkataba
   b. suala lolote la sheria ya kimataifa
   c. kuwepo kwa jambo lolote ambalo kama

litathibitishwa, linaweza kuathiri jukumu lolote la kimataifa.

d. hali au kiwango cha kurekebisha jukumu la kimataifa lililoathiriwa.

3. Maazimio yaliyoelezwa hapo juu yanaweza kutekelezwa bila masharti yoyote au kwa masharti kwamba sehemu au baadhi ya mataifa yanatekeleza maazimio hayo au yanatekelezwa katika kipindi fulani.
4. Maazimio kama hayo yatawekwa chini ya udhamini wa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa ambaye atatoa nakala ya udhamini huo kwa pande zinazohusika na sheria za sasa za Mahakama kwa Msajili wa Mahakama.
5. Maazimio yaliyofikiwa chini ya Ibara ya 36 ya sheria za Mahakama ya Kudumu ya Kimataifa na ambayo bado yanatekelezwa, kati ya pande zinazohusika na sheria za sasa za Mahakama, yatahesabiwa kuwa yamekubaliwa yawekwe chini ya mamlaka ya Mahakama ya Kimataifa kwa kipindi ambacho yataendelea kutekelezwa kulingana na muda wa utekelezaji na masharti yake.
6. Kama kutatokea mgogoro kuhusu suala la kama Mahakama ina mamlaka juu ya maazimio hayo, suala hilo litatatuliwa na uamuzi wa Mahakama.

## Ibara ya 37

Pale ambapo Mkataba au makubaliano ambayo bado yanatumika yanahusisha suala ambalo liko katika Baraza la Usuluhishi lililoanzishwa na Umoja wa Mataifa au liko katika Mahakama ya Kudumu ya Kimataifa, suala hilo litapelekwa katika Mahakama ya Kimataifa na pande zote zinazohusika na Sheria za sasa za Mahakama.

## Ibara ya 38

1. Mahakama, ambayo kazi yake ni kutoa maamuzi kulingana na sheria ya kimataifa kwa migogoro kama hiyo ambayo imewasilishwa mbele yake, itazingatia: makubaliano ya kimataifa ya kijumla au maalum, yanayoweka sheria zinazotambuliwa na mataifa yanayopingana; utamaduni wa kimataifa ambao kwa kawaida unakubalika kama ni sheria; kanuni za kawaida za sheria zinazotambulika na mataifa yaliyostaarabika; kulingana na masharti yaliyomo katika Ibara ya 59, maamuzi ya Mahakama na mafunzo ya watu mashuhuri wenye sifa zinazotakiwa katika nchi mbalimbali ambao wanaweza kutumika kama njia nyingine ya kupata maamuzi ya kisheria.
2. Sharti hili halitaathiri mamlaka ya Mahakama katika kuamua kesi ya 'ex aequo et bono' kama pande zinazohusika zitakubaliana.

## SURA YA III
# TARATIBU

### Ibara ya 39

1. Lugha rasmi za Mahakama zitakuwa ni Kifaransa na Kiingereza. Kama pande zitakubaliana kuwa kesi isikilizwe katika lugha ya Kifaransa, hukumu itatolewa katika lugha ya Kifaransa. Kama pande zitakubaliana kuwa kesi isikilizwe katika lugha ya Kiingereza, hukumu itatolewa katika lugha ya Kiingereza.
2. Pale panapokuwa hakuna makubaliano juu ya lugha ipi itumike, kila upande katika utetezi itatumia lugha ambayo itaipendelea, na maamuzi ya Mahakama yatatolewa katika lugha ya Kifaransa na Kiingereza. Katika suala hili Mahakama itaamua nakala zipi kati ya lugha hizo mbili itakuwa yenye mamlaka.
3. Mahakama kwa ombi kutoka upande mmojawapo, itaamuru lugha ipi zaidi ya Kifaransa na Kiingereza itumiwe na upande huo.

### Ibara ya 40

1. Kesi zinafikishwa Mahakamani kulingana na hali ama kwa kupeleka makubaliano maalum au kwa ombi la kimaandishi analopelekewa Msajili. Kwa

njia yoyote ile kiini cha mgogoro na pande zinazohusika zitatajwa.

2. Msajili baadaye atawasiliana na wahusika juu ya ombi hilo.
3. Atawataarifu pia Wanachama wa Umoja wa Mataifa kupitia Katibu Mkuu, na pia mataifa mengine ambayo yatatakiwa kufika mahakamani.

## Ibara ya 41

1. Mahakama itakuwa na mamlaka kuonyesha, kama itaona ni muhimu, hatua za muda inazotarajia kuchukua kulinda haki za kila upande.
2. Kabla ya maamuzi ya mwisho, taarifa ya hatua zilizopendekezwa itapelekwa kwa pande husika na kwa Baraza la Usalama.

## Ibara ya 42

1. Pande zote zitawakilishwa na wakala.
2. Zinaweza kupata msaada wa ushauri au wakili Mahakamani.
3. Wakala, washauri na mawakili wa pande zote waliofika Mahakamani watafaidika na haki muhimu ya kuendesha shughuli zao kwa uhuru.

## Ibara ya 43

1. Utaratibu utajumuisha sehemu mbili: Kimaandishi na Kimatamshi.

2. Uendeshaji wa kesi kimaandishi utajumuisha kuwasilisha Mahakamani na kwa pande zinazohusika kumbukumbu mbalimbali zinazodai na kupinga na kama ikilazimu majibu yake na nyaraka zote zinazounga mkono.
3. Mawasiliano haya yatapitia kwa Msajili, kulingana na utaratibu na katika muda uliopangwa na Mahakama.
4. Nakala iliyothibitishwa ya kila nyaraka inayotolewa na upande mmoja itawasilishwa kwa upande mwingine.
5. Uendeshaji wa kesi kimatamshi utajumuisha Mahakama kusikiliza mashahidi, wataalamu, mawakala, washauri na mawakili.

**Ibara ya 44**

1. Katika kuwasilisha nyaraka kwa watu ambao siyo mawakala, washauri na mawakili, Mahakama itaomba kibali kutoka kwa serikali ya nchi ambayo nyaraka hiyo inapelekwa.
2. Masharti hayo hayo yatatumika wakati wowote ambapo hatua zinachukuliwa kupata ushahidi mara moja.

**Ibara ya 45**

Kesi itaendeshwa chini ya usimamizi wa Rais wa Mahakama, au kama hawezi, chini ya Makamu wa

Rais au kama wote hawawezi, chini ya Jaji Mfawidhi atakayekuwepo.

**Ibara ya 46**

Kusikilizwa kwa kesi mahakamani kutakuwa wazi kwa hadhara, mpaka Mahakama iamue vinginevyo au mpaka pande husika ziamue kutoruhusu watu kuingia Mahakamani.

**Ibara ya 47**

1. Muhtasari utaandikwa kila baada ya kesi inaposikilizwa na kuwekwa saini na Msajili na Rais wa Mahakama.
2. Muhtasari huu pekee utakuwa sahihi.

**Ibara ya 48**

Mahakama itatoa amri ya kuendesha kesi, itaamuua utaratibu upi utumike na muda utakaotumika kwa kila upande kuhitimisha maelezo na kuweka mipango inayohusu uchukuaji wa ushahidi.

**Ibara ya 49**

Mahakama hata kabla ya kuanza kusikiliza kesi, inaweza ikawaita mawakala kutoa taarifa au kutoa maelezo yeyote. Taarifa rasmi ya kukataa taarifa yoyote itakubalika.

**Ibara ya 50**

Mahakama katika muda wowote inaweza ikamwamini mtu yeyote, chombo, ofisi, tume au

shirika jingine ambalo litachaguliwa kufanya jukumu la kuchunguza au kutoa ushauri wa kitaalamu.

**Ibara ya 51**

Wakati wa kusikiliza kesi, maswali yanayohusika yataulizwa mashahidi na wataalamu chini ya masharti yaliyowekwa na Mahakama katika kanuni na taratibu zinazoelezwa katika Ibara ya 30.

**Ibara ya 52**

Baada ya Mahakama kupokea vithibitisho na ushahidi katika muda uliowekwa kwa madhumuni hayo, inaweza kukataa kupokea ushahidi zaidi wa maneno au wa kimaandishi ambao upande mmoja unataka kuutoa mpaka upande mwingine ukubali.

**Ibara ya 53**

1. Pale ambapo upande mmoja haufiki Mahakamani, au unashindwa kujitetea katika kesi inayoukabili, upande mwingine unaweza kuiomba Mahakama kutoa maamuzi kulingana na madai yake.
2. Mahakama kabla ya kufanya hivyo, lazima iridhike yenyewe kuwa siyo tu ina mamlaka kulingana na Ibara za 36 na 37 bali pia madai hayo yana misingi ya ukweli na sheria.

**Ibara ya 54**

1. Wakati kulingana na mamlaka ya Mahakama; mawakala, washauri na mawakili wamemaliza kuwakilisha hoja zao za kesi, Rais wa Mahakama

atatangaza kuwa kusikilizwa kwa kesi kumemalizika.

2. Mahakama itaahirishwa ili ifikirie hukumu.
3. Mashauri ya Mahakama yatafanywa kwa faragha na yatabakia ni siri.

## Ibara ya 55

1. Maswali yote yatatolewa uamuzi na majaji wengi waliopo.
2. Kama kura za majaji zitakuwa sawa, Raisi wa Mahakama au Jaji anayeshikilia nafasi yake atakuwa na kura ya mwisho.

## Ibara ya 56

1. Hukumu itatoa sababu zilizopelekea hukumu hiyo kutolewa.
2. Itajumuisha majina ya majaji ambao walishiriki katika kutoa uamuzi huo.

## Ibara ya 57

Kama hukumu haiwakilishi maoni ya majaji wote au sehemu ya majaji, Jaji yeyote ana haki ya kutoa hukumu iliyo tofauti.

## Ibara ya 58

Hukumu itatiwa saini na Rais au na Msajili. Itasomwa wazi Mahakamani, baada ya taarifa kutolewa mapema kwa mawakala.

## Ibara ya 59

Uamuzi wa Mahakama hauna nguvu isipokuwa kati ya pande zinazohusika na kuhusiana na kesi hiyo.

## Ibara ya 60

Hukumu ya Mahakama ni ya mwisho na haina rufaa. Kama kunatokea mgogoro kuhusu maana ya hukumu au kiwango cha hukumu, Mahakama itatoa tafsiri kwa upande utakaotaka.

## Ibara ya 61

1. Ombi la kupitia hukumu linaweza kufanywa pale tu ambapo ombi hilo lina misingi ya kugunduliwa kwa baadhi ya ukweli ambao ni muhimu ambao wakati wa kutoa hukumu haukujulikana na Mahakama na kwa pande unaotaka hukumu hiyo ipitiwe tena na kutojulikana kwa ukweli huo hakukusababishwa na uzembe.
2. Uendeshaji kesi ya kupitia tena hukumu utafunguliwa na hukumu ya Mahakama baada ya kugundua kuwa kuna ukweli mpya ambao unadhihirisha wazi kwamba kuna sababu ya kupitia tena hukumu na kuruhusu ombi la kupitia hukumu kwa msingi huo.
3. Mahakama inaweza kuhitaji makubaliano yaliyokwishafikiwa katika hukumu hiyo kabla kukubali kuendesha kesi ya kupitia hukumu.

4. Ombi la kurudia hukumu lazima lifanywe mapema katika muda wa miezi sita tokea kugunduliwa kwa ukweli huo mpya.
5. Hakuna ombi la kupitia upya hukumu linaloweza kufanywa baada ya miaka kumi kupita tangu tarehe ya hukumu.

## Ibara ya 62

1. Pale taifa linapoona kuwa maslahi yake ya kisheria yanaweza yakaathirika na uamuzi katika kesi, linaweza likapeleka ombi kwa Mahakama kuruhusiwa kuingilia kati.
2. Itakuwa ni juu ya Mahakama kuamua ombi hilo.

## Ibara ya 63

1. Pale ambapo kuna utata katika makubaliano ya kisheria yanayofanywa na mataifa mbali na yale yanayohusika katika kesi, Msajili atayataarifu mataifa hayo mapema.
2. Kila taifa lililotaarifiwa litakuwa na haki ya kuingilia kati uendeshaji wa kesi; lakini kama litatumia haki hii, uamuzi wa Mahakama utalihusu taifa hilo pia.

### Ibara ya 64

Mpaka pale itakapoamriwa vinginevyo na Mahakama, kila upande utalipa gharama zake.

## SURA YA IV

# MAONI YA USHAURI

### Ibara ya 65

1. Mahakama inaweza kutoa maoni ya ushauri juu ya suala lolote la kisheria baada ya kuombwa na chombo chochote kitakachopewa mamlaka ya kutoa ombi hilo kulingana na Mkataba wa Umoja wa Mataifa.
2. Maswali ambayo maoni ya ushauri wa Mahakama yataulizwa, yatawasilishwa Mahakamani kwa njia ya maandishi yenye taarifa sahihi ya swali ambalo linahitaji maoni ya ushauri na yataambatana na nyaraka zote zinazohusiana na swali hilo.

### Ibara ya 66

1. Msajili atatoa taarifa haraka ya ombi la maoni ya ushauri kwa mataifa yote yanayotakiwa kufikishwa Mahakamani.
2. Msajili pia kwa njia za mawasiliano maalum na za moja kwa moja, atatoa taarifa kwa taifa lolote linalotakiwa kufikishwa Mahakamani au shirika la kimataifa linalofikiriwa na Mahakama au kama hakuna kikao, Rais anafikiri kwamba anaweza kufikisha habari ya jambo fulani, kwamba

Mahakama iko tayari kusikiliza kesi katika kipindi hicho ambacho Rais amekitaja, kwa njia ya maandishi au matamshi ya hadhara, ambayo yatafanyika kwa lengo hilo, yaliyozungumzwa kwa ajili au taarifa ya matamshi yanayohusiana na suala hilo.

3. Pale ambapo taifa lolote linalotakiwa kufika Mahakamani linashindwa kupata mawasiliano maalumu yaliyoandikwa kulingana na aya ya pili (2) ya Ibara hii, taifa hilo linaweza kueleza nia yake ya kupeleka taarifa kimaandishi au kwa mdomo; na Mahakama itatoa uamuzi.
4. Nchi na mashirika yanapokuwa yamewakilisha taarifa ya maandishi au ya mdomo au zote, yataruhusiwa kutoa maoni yao kuhusiana na taarifa zilizotolewa na nchi au mashirika mengine katika muundo, kwa kiwango na katika kipindi ambacho Mahakama, au kinapokuwa kimeahirishwa Rais ataamua katika kila shauri. Msajili katika kipindi hicho atawasilisha taarifa zozote za aina hiyo kimaandishi kwa mataifa na mashirika yaliyotoa taarifa kama hizo.

**Ibara ya 67**

Mahakama itatoa maoni yake ya ushauri katika Mahakama ya hadhara, taarifa ikiwa imepelekwa kwa Katibu Mkuu na kwa wawakilishi wa Wanachama wa Umoja wa Mataifa, wa mataifa mengine na wa mashirika ya kimataifa yanayohusika mara moja.

**Ibara ya 68**

Katika zoezi zima la kutoa ushauri, Mahakama itaongozwa na makubaliano yaliyopo katika Sheria za sasa ambazo zinatumika katika kesi zinazopingana kwa kiwango ambacho itaona inafaa.

## SURA YA V

# MAREKEBISHO

### Ibara ya 69

Marekebisho ya sheria hizi yataufata taratibu zilezile ambazo zimetajwa ndani ya Mkataba wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya marekebisho ya Mkataba huo, lakini yatazingatia maamuzi ya Baraza Kuu kutokana na mapendekezo ya Baraza la Usalama yanaweza kukubaliwa na mahudhurio ya mataifa ambayo ni sehemu ya Sheria za sasa lakini siyo Wanachama wa Umoja wa Mataifa.

### Ibara ya 70

Mahakama ina uwezo wa kupendekeza marekebisho hayo katika sheria hizi pale itakapoona ni muhimu, kupitia mawasiliano ya kimaandishi kwa Katibu Mkuu, kwa ajili ya kuyafikiria kulingana na makubaliano katika Ibara ya 69.